# Nipashe

Ijumaa Julai 31, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580298

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Lissu adaiwa kujiweka karantini, kesi zake kuendelea Agosti 26

UKURASA 2




UKURASA 11

# Msafara wa JPM waibua madudu

• **Ashangaa** DC, DED kukosa magari, soko kukosa choo, ambulensi kutofanya kazi, watoto waokoa shule kukarabatiwa, kupatiwa madawati... *Endelea ukurasa 2,3*



Rais John Magufuli akiwa na zawadi ya jogoo alilopewa na Shaweji Mohamed Kimbwembwe, mkazi wa Somanga mkoani Lindi jana, ambaye alifurahishwa na utendaji kazi wake wa kuwaletea maendeleo wananchi wanyonge. **PICHA: IKULU**

## Wajumbe wazidi kuwakata watiania wa ubunge vijana CCM

UKURASA 3

## TAKUKURU yamchunguza Gambo tuhuma za rushwa

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** **TSHISHIMBI AITINGISHA YANGA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Lissu ajiweka karantini, kesi zapigwa kalenda

**Na Hellen Mwango**

WAKATI Jeshi la Polisi likiwa limeimarisha ulinzi katika viunga vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, kesi mbili tofauti zinazomkabili Mbunge wa zamani wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, zimepigwa kalenda mpaka Agosti 26 mwaka huu baada ya utetezi kudai mshtakiwa huyo amejiweka karantini.

Kesi hizo jana ziliahirishwa mbele ya mahakimu wawili tofauti baada ya Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, kudai kuwa mshtakiwa ameshindwa kufika mahakamani kwa sababu ameshauriwa ajiweke karantini.

Katika kesi ya kwanza namba 123/2017, Lissu anakabiliwa na shtaka la uchochezi dhidi ya serikali, ikitajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Kassian Matembele.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Renatus Mkude, akisaidiana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, ulidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na mshtakiwa amesharejea nchini.

Wakili Kibatala pia alidai mshtakiwa amerejea nchini kutoka nje ya nchi, lakini ameshindwa kufika mahakamani kwa kuwa yuko karantini.

"Mheshimiwa hakimu, mshtakiwa ameshauriwa ajiweke karantini siku 14. Kwa hiyo, tunaomba tarehe nyingine ya kutajwa," Wakili Kibatala alidai bila kumtaja aliyemshauri mshtakiwa kukaa karantini. Baada ya maelezo hayo ya upande wa utetezi, Hakimu Matembele alisema kesi hiyo itatajwa Agosti 26 mwaka huu.

Katika ya msingi, Lissu anadaiwa kutoa maneno ya uchochezi wakati wa kampeni za uchaguzi mdogo wa Jimbo la Diman, Zanzibar, Januari 11, 2017, akiwa eneo la Kibunju Maungani, Wilaya ya Magharibi B, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Lissu alipandishwa kizimbani kwa mara ya kwanza Februari 9, 2017 na kusomewa mashtaka matano ya uchochezi, kutokana na maneno aliyodaiwa kuyasema siku hiyo.

Katika kesi ya pili, Makamu Mwenyekiti huyo wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo Taifa (CHADEMA), anakabiliwa na mashtaka matano ya kutoa lugha ya chuki dhidi ya serikali.

Kesi hiyo ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Agustina Mmbando.

Wakili Wankyo alidai mshtakiwa amerejea nchini, lakini hajafika mahakamani kwenye kesi yake wala wadhamini wake.

Kibatala alidai alijichanganya akawafahamisha wadhamini kufika mahakamani Jumatatu badala ya jana.

"Mheshimiwa, ninaomba radhi nimejichanganya nimewaeleza wadhamini waje Jumatatu badala ya leo (jana). Ninaomba radhi," alidai Kibatala.

Hakimu Mmbando alisema kesi hiyo itatajwa Agosti 26 mwaka huu na mshtakiwa asikose kufika mahakamani.

Katika kesi ya msingi namba 236/2017, Lissu anadaiwa kuwa Julai 17, 2017, akiwa eneo la Ufipa, Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam, alitoa maneno ya chuki.

Lissu anadaiwa kusema: "Serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Pombe Magufuli ni ya kibaguzi wa kifamilia, kikabila, kikanda na kidini. Vibali vya kazi 'work permits' vinavyotolewa kwa wamishenari wa kikatoliki tu huku madhehebu mengine yakielezwa kupanga foleni uhamiaji.

"Viongozi wakuu wa serikali wanachaguliwa kutoka kwenye familia, kabila na ukanda... Acheni woga pazeni sauti... kila mmoja wetu...tukawaambie wale ambao bado wanampa msaada wa pesa Magufuli na serikali yake kama tulivyoambiwa wakati wa serikali ya makaburu.

"Hii serikali isusiwe na jumuiya ya kimataifa, kisiasa, kiuchumi na kidiplomasia kwa sababu ya utawala huu wa kibaguzi... yeye ni dikteta uchwara."

Ilidaiwa kuwa maneno hao yalikuwa yana lengo ya kusababisha chuki.

Lissu alirejea nchini mwishoni mwa wiki baada ya kukaa ughaibuni kwa takriban miaka mitatu tangu aliposhambuliwa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana wakati akiwa kwenye gari lake nyumbani kwake jijini Dodoma mchana wa Septemba 7, 2017.



Rais John Magufuli akimkabidhi mwanafunzi wa Shule ya Msingi Somanga, Rehema Mikidadi Ngenje Sh. milioni 5 kwa ajili ya ukarabati wa shule hiyo, baada mwanafunzi huyo, kuelezea matatizo ya uchakavu wa shule hiyo. Rais aliagiza katika fedha hizo, mwanafunzi huyo apewe 100,000/-. **PICHA: IKULU**

# Msafara wa JPM waibua madudu

**Na Romana Mallya**

MSAFARA wa Rais John Magufuli mkoani Pwani umeibua madudu baada ya kuelezwa matatizo mbalimbali katika wilaya za Rufiji na Mkuranga, yakiwamo Mkuu wa Wilaya kukosa gari na wanafunzi kukaa chini madarasani licha ya serikali kuwekeza katika maendeleo ya elimu.

Sambamba na hayo, pia alishtushwa kuelezwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Juma Njwayo hana gari, magari ya kubebea wagonjwa ni bovu. Kutokana na matatizo hayo, ameagiza uchunguzi kufanyika huku akiwataka baadhi ya mawaziri kufika wilayani humo ili kujua chanzo cha matatizo hayo.

Magufuli alikumbana na mambo hayo jana alipokuwa njiani kwenda Dar es Salaam akitokea Lupaso, Masasi mkoani Mtwara alikokwenda kuongoza maziko ya Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, yaliyofanyika juzi.

Katika msafara huo, Rais Magufuli alisimama katika maeneo mbalimbali kusalimia wananchi na kuzungumza nao pamoja na kusikiliza kero mbalimbali. Miongoni mwa maeneo aliyotembelea ni Somanga, Kilwa mkoani Lindi, Ikwiriri na Utete wilayani Rufiji na Mkuranga mkoani Pwani.

Alipofika Ikwiriri alibaini kuwa kituo cha afya hakina gari la kubebea wagonjwa na alipohoji aliambiwa kwamba ni bovu pamoja na maeneo mengine ya wilaya hiyo.

Mmoja wa wananchi alimweleza Rais kuwa wilaya nzima haina gari la kubeba wagonjwa na kwamba yote ni mabovu na wanategemea ya wilaya ya Kibiti, iliyoanzishwa miaka kadhaa iliyopita baada ya kugawanywa kwa wilaya ya Rufiji.

Baada ya kuelezwa kero hiyo, aliwahoji viongozi wa eneo hilo akiwamo Mkuu wa Wilaya, Juma Njwayo na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ambao kwa nyakati tofauti walitolea ufafanuzi.

Kaimu Mkurugenzi alisema halmashauri ina magari manne ambayo ni mabovu lakini si kwa kiasi cha kushindwa kufanya kazi. Alisema gari la Ikwiriri liko katika matengenezo na tayari wameshatenga fedha kwa ajili ya kazi hiyo.

Baada ya maelezo hayo, Rais alitaka kujua kama kaimu mkurugenzi huyo ana gari na kubaini naye hana na mkurugenzi ambaye yupo safarini jijini Dar es Salaam analo ingawa nalo lina matatizo.

Rais Magufuli alielezwa kuwa katika wilaya hiyo mwenye gari ni Katibu Tawala wa Wilaya (DAS) lakini viongozi wengine hawana na Mkuu wa Wilaya hutumia hilo la DAS.

Baada ya maelezo hayo, Rais Magufuli alishangaa kwa nini tatizo hilo lipo licha ya wilaya kukusanya mapato lakini gari la kubeba wagonjwa ni bovu.

Njwayo alisema gari alilokuwa akilitumia limetembea zaidi ya kilometa 300,000 na kwamba mwezi mmoja baada ya kuteuliwa alipata nalo ajali na kufanyiwa matengenezo yaligharimu Sh. milioni 28 na baada ya muda likasimama.

Kutokana na maelezo hayo Rais Magufuli alisema amesikia na kuyaelewa matatizo yote na kuahidi kuyafanyia kazi huku akiahidi kutuma mawaziri wa sekta husika waende kuyashughulikia.

"Nimeona zipo changamoto nyingi za wakulima na wafugaji zipo za viongozi wenu hawana magari nitakwenda kuangalia kwa waziri wa TAMISEMI nijue katika halmashauri hii kuna magari mangapi.

Nataka nijua kwa nini DC (Mkuu wa Wilaya) hana gari wakati anatakiwa kutembelea maeneo na kutatua migogoro. Nitatuma watu wangu waje kufanya uchunguzi wa kutosha nijue tatizo ni nini. Yale nitakayoyaweza nitayatatua," alisema.

AMTAKA JAFO MKURANGA

Baada ya kufika Mkuranga, pamoja na mambo mengine, alishtushwa na taarifa kwamba hakuna kituo cha afya licha ya kwamba serikali ilishatoa Sh. milioni 400 kwa ajili ya ujenzi.

Kutokana na hali hiyo, alimpigia simu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwenda leo kuchunguza kwa nini kituo hicho hakijajengwa.

"Nataka ufike kesho hapa ili upate majibu kwa nini hakuna kituo cha afya. Nataka uhoji fedha zimekwenda wapi na kama zimeliwa ni nani aliyekula," alisema.

## Wanafunzi waokoa shule kukarabatiwa, kupatiwa madawati

**Na Romana Mallya**

WANAFUNZI wa shule za msingi za Somanga, Kilwa mkoani Lindi na Ali Hassan Mwinyi wilayani Mkuranga, Pwani, wameokoa shule zao kukarabatiwa na kupatiwa madawati.

Watoto hao walimweleza jana Rais John Magufuli matatizo yanayozikumba shule hizo na kusababisha kiongozi huyo wa nchi kutoa Sh. milioni tano kwa kila moja kwa ajili ya kutatua kero hizo.

Akiwa Somanga akitokea Mtwara kwenda Dar es Salaam, Rais alielezwa na mwanafunzi wa darasa la nne kwamba shule hiyo ina upungufu wa madawati, uharibifu wa sakafu, mabati yamechakaa na rangi kufutika.

Baada ya maelezo hayo, Rais Magufuli aliguswa na kumwita mwanafunzi huyo na kumkabidhi kitita cha Sh. milioni tano huku akiagiza kati ya fedha hizo, mtoto huyo apewe Sh. 100,000 kutokana na ujasiri wake wa kuibua kero mbele yake.

"Ninatoa milioni tano lakini Sh. 100,000 ubaki nayo wewe. Sawa mwanangu? Njoo uipokee kabisa siku moja uwe Waziri au Rais. Akabidhiwe hiyo fedha yake akanunue sare za shule, viatu, huyu kijana ni baraka kubwa," alisema.

Akiwa bado eneo hilo, Rais Magufuli alikabidhiwa jogoo na mzee mmoja ambaye alitaka apelekwe kwa mama wa Rais ikiwa ni zawadi kwa kumzaa mtoto anayesikiliza wanyonge.

"Ninaomba nikamkamate umpelekee mama yako mzazi aliyekufundisha vizuri, wema na huruma kwa wanadamu. Mpelekee mama hii ni zawadi kutoka kwa wananchi wa Somanga namna alivyokulea," alisema.

Baada ya maelezo hayo, Rais alimruhusu mzee huyo kwenda nyumbani kumchukua jogoo huyo na kwenda kumkabidhi Rais Magufuli, ndipo naye alipopewa zawadi ya Sh. 100,000 na Rais.

Akiwa Mkuranga, alielezwa na mwanafunzi mwingine kuwa wanakaa sakafuni kutokana na shule yao kukosa madawati, ndipo alipohoji gharama ya samani hizo na kuambiwa ni Sh. milioni saba.

"Haiwezekani shule yenye jina la Rais mstaafu wa Awamu ya Pili (Mzee Ali Hassan Mwinyi) kutokuwa na madawati. Mimi hapa natoa Sh. milioni tano na zingine wewe Mkurugenzi (Mtendaji) na Mbunge wa zamani, Abdallah Ulega (Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi), mchangie zilizobaki," alisema.

Ulega alipopewa nafasi aliahidi kuwa atachangia kiasi kilichobaki (Sh. milioni mbili) na kwamba atazikabidhi kesho.

# TAKUKURU yamchunguza Gambo

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Arusha, imesema inachunguza malalamiko iliyopokea kuhusu tuhuma za rushwa zinazomkabili aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo.

Alisema taasisi hiyo pia imejipanga vizuri kuhakikisha inadhibiti rushwa hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani uliopangwa kufanyika Oktoba 28 mwaka huu.

Vilevile, taasisi hiyo inamchunguza mfanyabiashara Philemon Mollel, kwa tuhuma za kujihusisha na rushwa wakati wa mchakato wa kura za maoni za kusaka kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwania ubunge wa Jimbo la Arusha Mjini katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu.

Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Arusha, James Ruge, alibainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana.

Kiongozi huyo wa TAKUKURU alisema: "Katika kipindi cha uchaguzi wa kura za maoni za Chama Cha Mapinduzi (CCM), tumekamata wagombea zaidi ya 20 ambao tunaendelea na uchunguzi dhidi yao.

"Kuna taarifa zilikuwa kwenye mitandao kuwa tumemkamata na Mrisho Gambo. Ninaomba nifafanue la Mrisho Gambo, hatujamkamata wala hatujamwita hapa ofisini kwetu kuhojiwa, ila kuna malalamiko yaliletwa na tunaendelea kuyafanyia uchunguzi na pindi uchunguzi ukikamilika kwa wote na kubainika kuwa walihusika, sheria itafuata mkondo wake," alisema.

Gambo na Mollel ni miongoni mwa makada wa CCM waliojitosa kuomba ridhaa ya chama hicho kuwania ubunge wa Arusha Mjini, Gambo akiongoza kwa kura 333 dhidi ya 68 za Mollel aliyeshika nafasi ya pili.

Ruge alivitaka vyama vya siasa vyenye nia ya kusimamisha wagombea katika uchaguzi mkuu ujao, kuhakikisha wagombea wake wana sifa stahili ili kuwapa wapigakura urahisi wa kuchagua kiongozi bora pasipokurubuniwa kwa rushwa.

Katika hatua nyingine, TAKUKURU Mkoa wa Arusha imeokoa Sh. bilioni 1.7 za kodi ya serikali na fedha za vyama vya ushirika baada ya kufanya operesheni katika kipindi cha kuanzia Aprili hadi Juni mwaka huu.

Pia, imeokoa Sh. milioni 190.164 za wajasiriamali sita wa Jiji la Arusha walizokuwa wamedhulumiwa na wamiliki wa kiwanda cha Kijenge Animal Products Limited.

Ruge alisema taasisi hiyo imefanya operesheni mbalimbali na kufanikisha kurejesha kodi ya serikali iliyokuwa haijalipwa na kampuni ya kitalii na uwindaji ya Eshkesh Safari na fedha za Chama cha Ushirika cha ACU (Arusha Cooperative Union) zilizokuwa hazijalipwa kwa chama baada ya mauzo ya mali za ushirika Sh. bilioni 1.765.

Alibainisha kuwa kiasi cha Sh. bilioni 1.484 ni kodi ya serikali iliyotokana na mizigo mbalimbali ambayo ilikuwa haijalipiwa na kampuni ya uwindaji na utalii ya Eshkeshi ya jijini Arusha, Sh. milioni 200 ni sehemu ya Sh. 904 za ACU zilizokuwa zimefanyiwa ubadhirifu baada ya mali za chama hicho kuuzwa kwa watu wasio waaminifu na Sh. milioni 45.448 ni fedha za vyama vya msingi vya ushirika, posho zilizolipwa zaidi ya stahili na fedha za makusanyo ya halmashauri ambazo hazikuwasilishwa kwenye akaunti za halmashauri husika.

Katika tukio lingine, TAKUKURU imefanikiwa kumrejeshea mfanyabiashara Advera Kyaruzi kiasi cha Sh. milioni 5.48 ambazo ni sehemu ya Sh. milioni 15 alizodhulumiwa na wafanyabiashara wenzake Gervas Andera Mollel na Joseph Chirstopher Mollel tangu mwaka 2018.

Kiongozi huyo wa TAKUKURU alisema kuwa, fedha hizo zilikuwa za mzigo wa biashara uliotapeliwa na Hervas na wenzake na kwamba taasisi hiyo inaendelea na uchunguzi kuhakikisha fedha zilizobaki zinalipwa na



Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) Mkoa wa Arusha, James Ruge (kushoto), akikabidhi fedha Sh. millioni 235 kwa Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Mkoa huo (ACU), Shedrack Isanja, jijini Arusha jana, ambazo zilikuwa hazijalipwa kwa chama hicho, kutoka kwa wanunuzi, baada ya mauzo ya mali za ushirika. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wajumbe waendelea kukata watiania CCM

**Na Waandishi Wetu**

WAJUMBE wa mkutano mkuu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), walikutana katika mikoa mbalimbali nchini jana na kupiga kura kuwapata wabunge wa viti maalum kupitia umoja huo.

Mkoani Iringa, wajumbe walimpigia kura nyingi mwanahabari Secky Kasuga aliyekuwa amejitosa kuwania nafasi sita za kitaifa za ubunge viti maalum kupitia kundi la vijana wa UVCCM Tanzania Bara.

Katika mchuano huo uliokuwa umevutia makada 13, Kasuga aliongoza baada ya kupata kura 12, akifuatwa na Agape Mahenge (8) na Zawadi Amri (7).

Halima Bulembo aliongoza kura hizo mkoani Kagera, akiwazidi kete makada 18 baada ya kupata kura 35 kati ya 48 zilizopigwa, akifuatwa na Joanfaith Kataraia (9) na Koku Ruta (2).

Mkoani Kilimanjaro, Agnes Mchau aliongoza kwa kupigiwa kura 24 akifuatwa na Rusma Ndosi (7), Jesca Ngowi, Mercy Lyimo na Godness Kwayu waliopata kura mbili kila mmoja.

Makao makuu ya nchi mkoani Dodoma, Monishaz Mazanda aling'ara kwa kura 15 akifuatwa na Jesca Mshama (8) na Salome Komba (7).

Azmina Amir aliongoza kwa kura 13 mkoani Shinyanga akifuatwa na Janeth Dutu aliyepigiwa kura sita na Leah Mbeke aliyepata kura tano.

Kwa mujibu wa Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa, Oganaizesheni ya CCM, Pereira Silima, baada ya kura hizo za maoni, Agosti 8 hadi 10 mwaka huu, itakuwa ni mchujo wa wagombea wa jumuia zote waliopitishwa kila mkoa.

"Na wagombea wote walioshinda katika jumuiya hizo watapigiwa kura ya pamoja na Baraza Kuu la kila jumuiya na watakaoshinda ndiyo watakuwa wagombea na watachukuliwa mmoja kila mkoa,"alisema Silima.

"Mtu ambaye atakuwa amekiuka maadili na mambo mengine atashughulikiwa kwa sababu katika mchakato huu vinaangaliwa vigezo vingi ikiwamo kura alizopata, sifa zake kichama na kijamii na mambo mengine."

■**Imeandikwa na Mary Mshami (DAR), Francis Godwin (IRINGA), Allawi Kaboyo (BUKOBA).**

MAKALA MAALUM

# NIC yachekelea umri miaka 50 na bima mpya mkononi

## ■Mkurugenzi: Wakulima, wajasiriamali tunao rasmi

Na Enock Charles

WAKATI taifa likiadhimisha miaka zaidi ya 50 ya huduma za bima nchini, sekta hiyo imeendelea kukua na kupata mafanikio zaidi licha ya kuwapo kwa vikwazo kadhaa, huku ikiibua aina mpya za bima.

Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, Mamlaka ya Usimamizi ya Bima na wadau wa sekta hiyo, imetoa mchango mkubwa katika kuhakikisha sekta ya bima inakuwa na mafanikio na kuchangia ukuaji wa uchumi wa taifa.

Mchango huo umefanya baadhi ya kampuni na mashirika ya bima kuwa wabunifu na kuja na bidhaa mbalimbali za bima ambazo zinawapa wananchi uwanja mpana wa kuchagua huduma.

Miongoni mwa bidhaa za bima zinazoonekana kuleta tija katika nyanja za maendeleo nchini, ni bima ya kilimo na bima nyingine kwa wajasiriamali wadogo na wa kati zinazotolewa na Shirika la Bima la Taifa (NIC).

Kaimu Mkurugenzi wa Bima za Mali na Shehena wa NIC, Ntimba Bunny, anasema shirika hilo la umma limeamua kuwasaidia Watanzania kujikwamua kutoka kwenye lindi la umaskini kupitia bidhaa bora za bima zinazoendana na kipato chao halisi.

Anasema bima hizo zinawasaidia wajasiriamali wa Tanzania si tu kuepukana na majanga, bali kukopesheka katika taasisi za kifedha na kuwa na uhakika wa kukuza biashara zako.

"Wajasiriamali wadogo na wa kati ni kundi muhimu katika juhudi za kufikia mapinduzi ya kiuchumi nchini. Kundi hili ni msingi mkuu wa kuwa na viwanda vikubwa. Kwa kutambua umuhimu wa makundi haya, NIC tumeamua kuja na bidhaa za bima kwa lengo la kutoa ulinzi kwenye shughuli za watu hawa," anasema Bunny.

Anasema NIC inatambua fika kwamba makundi hayo yanafanya shughuli mbalimbali za uzalishaji mali kwa lengo la kujipatia kipato na kutoa ajira kwa kutumia mikopo kutoka kwenye taasisi ya fedha, hivyo shughuli zao zinahitaji ulinzi wa bima pindi janga linapotokea.

**BIMA ZA SACCOS**

Bunny anasema NIC inatoa bidhaa nyingi za bima kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kwa lengo la kulinda mali zao, ikiwa ni pamoja na bima za vikundi vya kuweka na kukopa (SACCOS).

Anasema katika kundi hilo, NIC imeamua kuja na bidhaa ya bima kwao kwa lengo la kulinda fedha za wanakikundi, akifafanua kuwa kuna wakati inatokea mwanakikundi anafariki dunia au upotevu wa fedha kwenye kikundi hicho kutokana na sababu mbalimbali, hivyo bima hii inafidia hasara iliyojitokeza.

**BIMA ZA MOTO**

Bunny anasema bima ya moto inalipia hasara iliyopatikana kutokana na majanga yanayosababishwa na ajali ya moto, radi au milipuko na kwamba inahusisha mali iliyokatiwa bima eneo lolote kwa mujibu wa taarifa iliyoko katika maelezo ya bima ya awali.

"Pia inahusisha moto na majanga mengine kama vile kutokana na sababu za kiufundi au majanga yanayosababishwa na umeme, bima hii inawasaidia wajasiriamali wadogo na wa kati kulinda biashara zao dhidi ya hasara zitokanazo na majanga haya," anasema.

**BIMA ZA MAGARI**

Kaimu Mkurugenzi huyo anasema NIC inatoa huduma bora kwa bima ya magari na kwa watu wenye vyombo vya usafiri vya thamani, ili kuwalinda dhidi ya hasara itakayosababisha uharibifu wa gari lililopata ajali, wizi, au moto.

Anasema aina hiyo ya bima inalipa hasara inayosababishwa na matukio ya moto, wizi, ajali kwa kugongana au kupinduka na matukio mengine yanayokusababisha hasara katika gari lililokatiwa bima ya aina hiyo.

**BIMA YA AJALI BINAFSI**

Bunny anasema bima ya ajali binafsi inazingatia ukweli kwamba ukiwa katika shughuli zako za uzalishaji, kunakuwa na uwezekano mkubwa wa kupata ajali na kukusababisha madhara mwilini.

Anafafanya kuwa gharama za matibabu kwa ajali ya aina hiyo huenda zikawa tatizo kubwa, hivyo wakaona hakuna haja ya mtu kubeba mzigo huo peke yake na NIC wameliona hilo kwa kugharamia matibabu, ulemevu uliyosababishwa na ajali na gharama nyingine endapo zikitokea.

BIMA YA MKOPO

Kaimu Mkurugenzi huyo anasema wajasiriamali wengi wanapata misingi ya biashara kutokana na mikopo kutoka kwenye taasisi za kifedha.

Kwa kulitambua hilo, NIC ina bima ya suala hilo ambayo inalipia hasara ya fedha anayoipata mkopeshaji kutokana na matatizo aliyopata mkopaji kupitia majanga ya kifo au ulemavu wa kudumu kabla hajamaliza kulipa deni, ili kusaidia kupunguza hasara ikilinganishwa na dhamana iliyowekwa.

"Bima hii inahakikisha familia ya mwathirika haiachwi bila makazi au mzigo wa kuendelea kulipa deni linalodaiwa," anasema Bunny.

**BIMA YA UAMINIFU**

Kiongozi huyo wa NIC anasema bima ya uaminifu inalinda biashara au mali ya mtu kutokana na wizi uliosababishwa na uaminifu, akifafanua "Mfano, mjasiriamali akiwa amemwajiri mtu kusimamia biashara yake, halafu kumsababishia mwajiri wake hasara, bima hii inalipa fidia kwa hasara hiyo."

Bunny pia anasema NIC ina bima ya usafiri wa maji na uvuvi ambayo hukatwa kwa ajili ya kulipia hasara inayopatikana kwa mali zinazosafirishwa kwa njia ya baharini.

Vilevile, Kaimu Mkurugeni huyo anasema wana bima ya mazao ambayo Ofisa Bima wa shirika hilo, Prosper Peter, anasema inawasaidia wakulima katika nyanja tofauti.

Peter anasema bima ya mazao inamsaidia mkulima kujikinga na majanga yanayoweza kusababisha uharibifu wa mazao kama vile mafuriko, tetemeko la ardhi na mabadiliko ya tabianchi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima la Taifa (NIC), Dk. Elirehema Doriye.

**BIMA YA VIWANDA**

Kwa kutambua kuwa kwa sasa Tanzania ni nchi yenye uchumi wa kati unaochagizwa na viwanda, Buuny anasema NIC inatoa bima ya viwanda na ina uwanja mpana wa kulipa fidia ya hasara kuliko bima ya moto ya kawaida.

"Bima hi inatoa kinga dhidi ya majanga mbalimbali kama vile moto, wizi, ajali, hasara za matatizo ya biashara pamoja na hatari nyingine zinazoweza kutokea katika shuhuli za viwandani," anasema.

Bunny anafafanua kuwa, bima ya viwanda ya NIC imegawanyika katika maeneo makuu mawili ambayo ni uharibifu wa mali na matatizo ya kibiashara.

Katika uharibifu wa mali, kiongozi huyo wa NIC anasema bima yao inashughulikia ulipaji wa fidia kutokana na uharibifu wa mali na vifaa mbalimbali kiwandani, ikiwa ni pamoja na kuharibika kwa mashine iliyokatiwa bima.

Kwa upande wa matatizo ya kibiashara, anasema bima yao inashughulikia hasara zinazotokana na matatizo ya kibiashara yaliyosababishwa na majanga ya moto na kuathiri uzalishaji kiwandani, na pia fidia ya kiwanda kushindwa kutengeneza faida kutokana na kuharibu kwa mashine ya uzalishaji.

Bunny anasema wajasiriamali na wakulima wamepata faraja kwa uanzishwaji wa bidhaa hizo za bima kwa kuwa kwa muda mrefu wamekuwa wakipambana na vikwazo vingi katika shughuli zao bila kupata suluhisho.

"Mwamko ni mkubwa na kuridhisha sana. Tunawaomba Watanzania kuja kukata bima NIC kwa sababu bima ni kitu muhimu na umuhimu wake huonekana pale ambapo janga limetokea. Lengo la bima ni kumrudisha mtu ama biashara katika hali yake ya kawaida baada ya majanga," anasisitiza.

TANGAZO

# VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LIMITED

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA WA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka ya sasa Tarehe 30/06/2020 | Robo ya Mwaka iliyopita Tarehe 31/03/2020 |
|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS |
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 110 | 60 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 13,688 | 9,135 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushungulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima ya Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa Kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | | - | - |
| | Mikopo Halisi Iliyopo | 13,664 | 18,937 |
| 12 | Mali Nyingine | 3,761 | 3,103 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika ,Mitambo na Vifaa | 1,828 | 1,896 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **33,052** | **33,131** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 1,439 | 1,818 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 3,453 | 4,090 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 563 | 328 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 702 | 214 |
| 27 | Zitakazolipwa Baadae | 2,075 | 1,057 |
| 28 | Dhima Nyingine | - | - |
| **29** | **Madeni** | **8,232** | **7,507** |
| | **JUMLA YA DHIMA** | | |
| **30** | **MALI/(DHIMA)HALISI (16 kutoka 29)** | **24,819** | **25,625** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,200 | 21,200 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 12 | 12 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 1,679 | 1,835 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (265) | 12 |
| 35 | Akauti Nyingine za Mtaji | 2,194 | 2,566 |
| 36 | **Stahiki ya Wenyehisa Chache** | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISANI** | **24,819** | **25,625** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 | Mikopo Chechefu | **1,640** | **1,640** |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | **1,755** | **1,437** |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | **75%** | **77%** |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | **15.3%** | **8.2%** |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | **305%** | **345%** |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Hali na Mali | **45%** | **61%** |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | **53%** | **66%** |
| (vi) | Ongezeko la Amana | **-17.2%** | **-1.3%** |
| (vii) | Ongezeko la Mali | **-0.2%** | **0.5%** |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 JUNI 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa Tarehe 30/06/2020 | Robo ya Mwaka Linganishi 30/06/2019 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/06/2020 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30/06/2019 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS | TZS | TZS |
| 1 | Mapato ya Riba | 2,356 | 3,091 | 5,156 | 6,092 |
| 2 | Gharama za Riba | 4 | 108 | 7 | 208 |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2 )** | **2,353** | **2,983** | **5,149** | **5,884** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (494) | **65** | (674) | **(176)** |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **394** | **476** | **870** | **995** |
| | 6.1 Faida/(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (0) | (2) | (0) | (1) |
| | 6.2 Ada za Kamisheni | 213 | 368 | 573 | 791 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 181 | 110 | 297 | 205 |
| **7** | **Gharama Zisizo na Riba :** | **2,530** | **3,185** | **5,610** | **6,373** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 1,320 | 1,670 | 2,886 | 3,334 |
| | 7.2 Gharama Nyingine | 1,210 | 1,515 | 2,725 | 3,039 |
| | 7.3 Ada na Kamisheni | | | | |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(277)** | **340** | **(265)** | **331** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| **10** | **Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(277)** | **340** | **(265)** | **331** |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | **292** | **349** | **292** | **349** |
| 12 | Mapato kwa Hisa | (13,069) | 16,024 | (13,005) | 16,211 |
| 13 | Kipato kwa Hisa | (13,069) | 16,024 | (13,005) | 16,211 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| 15 | Vituo Vya Biashara | 53 | 54 | 53 | 54 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Mapato na Wastani wa Mali | -0.8% | 0.9% | -0.7% | 0.9% |
| (ii) | Uwiano wa Mapato na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -1.1% | 1.3% | -1.1% | 1.4% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 92% | 92% | 93% | 93% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani Wa Mali Zinazozalisha | **22%** | **23%** | **35%** | **40%** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 30 JUNI 2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa Mwaka (2020)** | **21,200** | **1,657** | **190** | **2,566** | **25,613** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | **(265)** | - | - | **(265)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | **190** | **(190)** | - | - |
| Mengineyo | - | **(168)** | - | **(360)** | **(528)** |
| **Salio la mwisho wa Robo ya mwaka wa sasa** | **21,200** | **1,414** | **0** | **2,205** | **24,819** |
| **Salio la mwanzo wa Mwaka Uliopita ( 2019)** | **21,200** | **1,513** | **204** | **2,123** | **25,040** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | **529** | - | - | **529** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | **(385)** | **(14)** | **443** | **45** |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **21,200** | **1,657** | **190** | **2,566** | **25,613** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 JUNI 2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa Tarehe 30/06/2020 | Robo ya Mwaka iliyopita Tarehe 31/03/2020 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/06/2020 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30/06/2019 |
|---|---|---|---|---|
| | TZS | TZS | TZS | TZS |
| **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULI ZA UENDESHAJI** | | | | |
| Mapato/(Hasara)Hakisi | **(277)** | **12** | **(265)** | **340** |
| **Marekebisho kwa Ajili ya:** | | | | |
| Hasara Katika Mali | 115 | 121 | 237 | 125 |
| Badiliko Halisi Katika Mikopo | 5,273 | 608 | 5,881 | 1,568 |
| Faida/Hasira Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Amana | (1,016) | (76) | (1,092) | 337 |
| Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (658) | (108) | (766) | (184) |
| Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| Mengineyo | 1,741 | 220 | 1,961 | (327) |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | - | - | - | - |
| **kwa shughuli za uendeshaji** | **5,179** | **777** | **5,956** | **1,858** |
| **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTIKANA NA SHUGHULI ZA UWEKEZAJI** | | | | |
| Gawio Lililopokelewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (47) | (205) | (252) | (496) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za uekezaji** | **(47)** | (205) | (252) | (496) |
| | - | - | - | - |
| **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULIZA KIFEDHA** | - | - | - | - |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | (557) |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo | (528) | - | (528) | 106 |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | - | - | - | - |
| **kwa Shughuli za Kifedha** | **(528)** | **-** | **(528)** | **(451)** |
| **FEDHA TASLIMU NA MALI ZAINAZOFANANA NA FEDHA TASLIMU** | | | | |
| Onzezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofana na Fedha Tastimu | 4,603 | 572 | 5,176 | 911 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 9,195 | 8,622 | 8,622 | 9,350 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu / Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **13,798** | **9,195** | **13,798** | **10,261** |

Katika kuaandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Yohane Ibrahim Kaduma ( Ofisa Mtendaji Mkuu) | | 15 Julai 2020 |
| Rogathe Godson (Mkuu wa Fedha ) | | 15 Julai 2020 |
| Nuru Zakayo (Kaimu Mkaguzi mkuu wa Ndani) | | 15 Julai 2020 |

Sisi,tuliotajwa hapo chini,wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifaza zahapo juu,Tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **Mwijage B Bishota (Mwenyekiti ya Bodi)** | | 15 Julai 2020 |
| **Loyce Isanzu (Mwendeshaji)** | | 15 Julai 2020 |

## ADA NA GHARAMA

**Group Loans Product**

| | Product | Interest p.m. | VAT Inclusive Processing Fees |
|---|---|---|---|
| 1 | Group Biashara | 3% flat | 3% |
| 2 | Group Savings Group Loan | 3% flat | 2.5% |
| 3 | Group Jiendeleze | 2.5%flat | 3.5% |

**Individual Loans Product**

| | Product | Interest | Proc. Fee |
|---|---|---|---|
| 4 | Kitita | 2.5% flat | 2.5% |
| 5 | Premium | 2% flat | 2.5% |
| 6 | Uzalishaji | Btn 14% to 30% Declining balance and | 1.5% - 2.5% |
| 7 | Elimisha | 2.5% flat | 3.5% |

**Agriculture (Balloon) Loans Product**

| | Product | Interest | Proc. Fee |
|---|---|---|---|
| 9 | Jikomboe | 4% flat | 5% |
| 10 | Jitume | 5% flat | 5% |
| 11 | Mkombozi | 5% flat | 5% |

| | Product | Interest | VAT Inclusive Processing Fees |
|---|---|---|---|
| 12 | Partnership | Negotiable | Negotiable |

**Banking Services**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Balance Enquiry | n/a | Free |
| 2 | Dormancy Fees | n/a | 5000 pm |
| 3 | Payments | n/a | Free |
| 4 | Withdrawal | n/a | 300 |

**Mobile Banking**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4 | Balance Enquiry | n/a | Free |
| 5 | Payments | n/a | Free |
| 6 | Withdrawal | n/a | Free |

**Saving Products**

| | Product | Riba Kwa mwaka | VAT Inclusive Processing Fees |
|---|---|---|---|
| 1 | Savings Group Accounts | 4% | n/a |
| 2 | Joint Accounts | 4% | n/a |
| 3 | Akiba Accounts | 4% | n/a |
| 4 | Watoto Accounts | 4% | n/a |
| 5 | Bussiness Accounts | 4% | n/a |
| 6 | Fixed Deposit Accounts | Tied to the Amount | n/a |
| 7 | Conditional Savings | Tied to the Amount | n/a |

| Jina na cheo | Signature | Date |
|---|---|---|
| Yohane Ibrahim Kaduma ( Ofisa Mtendaji Mkuu) | Signed | 15 Julai 2020 |
| Rogathe Godson (Mkuu wa Fedha ) | Signed | 15 Julai 2020 |
| Nuru Zakayo (Kaimu Mkaguzi mkuu wa Ndani) | Signed | 15 Julai 2020 |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua alizochukua DC Muheza ni mfano wa kuigwa na viongozi, watendaji wa ngazi zote nchini

**TANGU** alipoingia madarakani Novemba 5, 2015 Rais John Magufuli amekuwa akiwateua watu kushika nafasi mbalimbali serikalini, huku akiwaagiza kwenda kushughulikia kero za wananchi katika maeneo yao.

Maagizo hayo ya Rais yamekuwa yakilenga viongozi hao kuwajibika katika majukumu yao ya kila siku kutokana na wananchi wengi kukumbwa na matatizo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Miongoni mwa kero hizo ni maji, migogoro ya ardhi, upungufu wa vyumba vya madarasa, madawati, nyumba za walimu na wananchi kudhulumiwa haki zao ikiwamo kudhulumiwa fedha za mazao yao kutoka kwa wafanyabiashara.

Kutokana na kero hizo, watendaji na viongozi wa kuchaguliwa kuanzia ngazi za vijiji hadi taifa, wamekuwa wakitakiwa kuchukua hatua katika kuzimaliza na zile zinazoshindikana kupelekwa ngazi za juu kwa utatuzi zaidi. Licha ya kutoa maagizo hayo, baadhi ya watendaji wamekuwa wakishindwa kutatua kero huku wengine wakijiingiza na kuwa sehemu za migogoro.

Hatua hiyo imesababisha baadhi yao kutumbuliwa na nafasi zao kuchukuliwa na watu wengine. Pamoja na Rais kuwatumbua baadhi ya watu hao, wako wengine ambao wamekuwa wakifanya vizuri na hatimaye kupewa nafasi za juu zaidi au kupewa pongezi kwa utendaji wao mzuri.

Miongoni mwa viongozi ambao wamekuwa wakijitahidi katika utatuzi wa kero na migogoro katika maeneo yao ya utawala ni Mkuu wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Mhandisi Mwanasha Tumbo.

Tangu kuteuliwa kwake mwaka 2016, kiongozi huyo amekuwa akishughulikia kero zinazohusu sekta mbalimbali kama vile afya, elimu, miundombinu. Moja ya kazi alizofanya na kusimamia hata kupewa sifa ni usimamizi wa ujenzi wa hospitali mpya ya wilaya. Kabla ya hapo, wilaya ilikuwa hospitali ya Kanisa la Anglikana kama hospitali teule.


Hivi karibuni, kiongozi huyo aliripotiwa kuwa amehamishia ofisi yake chini ya mti kwa ajili ya kusikiliza kero za wananchi na hatimaye kuzitafutia ufumbuzi kwa zile ambazo ziko chini ya uwezo wake na zingine kuziwasilisha sehemu husika ili kupata suluhisho.

Katika kufanya hivyo, Mhandisi Tumbo ametangaza kuwa kila Jumatano, ofisi yake itahamia chini ya mti kusikiliza matatizo ya wananchi na kila Jumanne, kukutana na wafanyakazi wa taasisi mbalimbali na watumishi wa umma ambao wanakabiliwa na matatizo mbalimbali.

Lengo la kufanya hivyo, kwa mujibu wa kiongozi huyo ni kuleta ufanisi katika utumishi wa umma na kuepusha migogoro kati ya waajiri na wafanyakazi. Utendaji huu unaopaswa kuigwa na kila mtu aliyepewa dhamana ya uongozi katika sehemu yake.

Ni hakika kwamba kama kila kiongozi atawajibika ipasavyo katika nafasi yake kuanzia ngazi ya mtaa au kitongoji, matatizo mengi yanayoikabili jamii yatapungua au kumalizika kabisa badala ya kusubiri viongozi wa kitaifa, akiwamo Rais, wanapofanya ziara za kikazi katika maeneo mbalimbali ya nchi kama ambavyo imekuwa ikishuhudiwa mara kwa mara.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Ujasiriamali chakula muhimu, lakini usafi mazingira lazima

**AFYA** ni kitu muhimu katika mwili wa mwanadamu. Ndilo linamhakikishia binadamu afya bora na amani.

Hapo ndipo kunazaliwa haja ya wajasiriamali chakula ambao ni wengi katika maeneo ya mijini na kokote kwenye shughuli za kijamii na kipato, mathalan stendi ya basi, panakotakiwa kuhakikishwa biashara inaandaliwa katika mazingira bora na salama.

Vitu vya usafi wa biashara vinaangaliwa sana na wataalamu wa masuala ya afya na lishe.

Hiyo inatokana na kujali afya za walaji na inapobainika kuna uchafu katika maeneo hayo wahusika wanapaswa kuchukuliwa hatua kama faini.

Ili mhusika asitozwe faini, sehemu ya vigezo vya kisheria anatakiwa azingatie suala la usafi katika maeneo yake ya biashara.

Si ajabu kukaguliwa maeneo mbalimbali, mtu atakuta baadhi hawazingatii kabisa suala la usafi.

Kutozingatia suala la usafi kunasababisha walaji wanaoendelea kula chakula na kuuzwa matunda ambayo yamekuwa yakilambwa. Si jambo jema.

Uhakikishaji afya za walaji zinakuwa salaam. Inatakiwa kuzingatia kanuni za usafi na inazingatia pande zote mbili, yaani mlaji na muuzaji.

Tunaposema mlaji tuna maana mlaji asile bidhaa yoyote inayofanyika katika mazingira machafu. Muuzaji naye hatakiwi kufanya biashara katika maeneo yasiyofaa.

**Katika mifumo yetu kijamii kumekuwapo mafunzo yanayotolewa kwa makundi hayo, ili kuhakikisha wanaandaa vyakula katika maeneo safi na salama, lengo likiwa ni kuwapatia walaji chakula kilicho salama na kisafi.**

Katika mifumo yetu kijamii kumekuwapo mafunzo yanayotolewa kwa makundi hayo, ili kuhakikisha wanaandaa vyakula katika maeneo safi na salama, lengo likiwa ni kuwapatia walaji chakula kilicho salama na kisafi.

Inapokuwapo ongezeko la biashara za bidhaa kama vyakula, matunda na kushuhudia wachoma nyama na mishikaki, baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakifanya biashara katika maeneo yasiyofaa.

Ni maeneo yanayokutwa na hitilafu kama mifereji ya majitaka na unakuta wafanyabiashara wa mishikaki, matunda na wauza samaki mbichi na za kukaanga wanaendelea kana kwamba hakuna kitu.

Tunapokuwa tunafanya biashara kuna mambo yasiyo sahihi. Kuna maeneo yanashangaza, bidhaa kama matunda yamepangwa katika meza.

Unaweza kushangaa chini ya eneo kuna mtaro wa maji machafu na yanayotoa harufu mbaya, isiyoendana na usafi ya mazingira.

Biashara inapofanyika upande wa pili wa shilingi, walaji nao wajali afya zao inakuwa hatarini. Biashara inafanyika katika mazingira yasiyofaa, hivyo kujali maslahi ya walaji.

Kwa kufanya hivyo wanaweza kuwasababishia walaji kupata ugonjwa wa tumbo kutokana na ulaji vitu vilivyoandaliwa katika mazingira yasiyofaa.

Niseme biashara ya mlo na usafi wa mazingira, ni jambo linaloendana kwa ubia. Ifanyiwe kazi.

# Magereza yaruhusu wafungwa kutembelewa kuanzia kesho

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

JESHI la Magereza nchini limesema kuanzia Agosti mosi, mwaka huu, litarejesha rasmi shughuli za kutembelea wafungwa na mahabusu na huduma mbalimbali magerezani kutokana na kupungua kwa kiasi kikubwa maambukizi ya virusi vya corona. Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Msemaji wa Jeshi la Magereza nchini SSP, Amina Kavirondo, alisema kufuatia kuripotiwa ugonjwa wa corona nchini Jeshi la Magereza lilisitisha huduma zote za kutembelea wafungwa na mahabusu ikiwamo za kupelekewa chakula.

"Hatua hii imekuja baada ya kushuka kwa kasi ya maambukizi Tanzania kwa kiasi cha kuridhisha na kwa kuzingatia tamko la Rais John Magufuli la kuzitaka taasisi mbalimbali za serikali kurejea katika shughuli za awali za utendaji kazi," alisema.

Alisema kuwa, Jeshi la Magereza linawataka wageni wote kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya Jeshi na Wizara ya Afya wakati wa upokeaji wa huduma hiyo.

Vile vile, alisema kuwa wageni watatakiwa kuzingatia mambo muhimu ikiwamo, mfungwa, mahabusu kutembelewa na ndugu wasiozidi wawili kati ya Jumamosi au Jumapili na mazungumzo yatatakiwa yasizidi dakika tano, na wenye vibali vya kuleta chakula italazimika kuletwa na mtu mmoja. "Mambo mengine ni pamoja na wageni wote wavae barakoa na kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni wanapoingia eneo la Gereza na wanapoingia gerezani, kuwa umbali wa mita moja kati ya mfungwa, mahabusu na mgeni lazima uzingatiwe na mazungumzo ya kisheria kati ya wakili na mteja wake yasizidi saa moja," alisema Kavirondo.

Alisema jamii inapaswa kujua hivi sasa masharti yamelegezwa na kuitaka kuzingatia kile kitakachotolewa na jeshi hilo. Kavilondo, alisema wameamua kufanya hivyo baada ya ugonjwa wa Covid -19, kupungua nchini.

Jeshi la Magereza liliweka katazo la raia kwenda kuona mahabusi kutokana na ugonjwa wa corona kuingia nchini na serikali kutoa tamko la kuzuia mikusanyiko.



Wafanyabiashara wa Mbuzi wakisubiri wateja katika mnada wa Vingunguti, jijini Dar es Salaam, jana. Kutokana na Sikukuu ya Idd El Haj kusherehekewa leo, bei ya kitoweo hicho, iliuzwa 120,000/- hadi 180, 000/- kwa mbuzi mmoja kulingana na ukubwa wake. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Polisi yaua watatu kwa tuhuma ujambazi

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limewaua watuhumiwa watatu wa ujambazi, huku mmoja akidaiwa kukutwa amevaa sare za jeshi hilo.

Kamanda wa Polisi wa kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, aliwaambia waandishi wa habari jijini jana kuwa watuhumiwa hao waliuawa eneo la Mbagala, Chamanzi jijini.

Alisema baada ya mashambulizi yaliyofanywa na polisi, katika upekuzi ndani ya gari lenye namba za usajili T 855 ATE aina ya Nissan X-Trail lililokuwa likitumiwa na watuhumiwa hao, mmoja alikutwa akiwa na sare za jeshi hilo.

Alisema tukio hilo lililotokea Jumapili usiku baada ya polisi kupata taarifa ya kuwapo kwa watu hao waliokuwa wanajipanga kufanya uhalifu maeneo hayo.

"Baada ya taarifa, kikosi cha kupambana na ujambazi kiliweka mtego eneo hilo na walipohisi wanafuatiliwa, ghafla walianza kupiga risasi ovyo na ndipo polisi walipojibu mapigo kulishambulia gari hilo," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema katika majibizano hayo, waliwaua watatu na mmoja alikimbia na walipofanya upekuzi kwenye gari hilo, mmoja wa watuhumiwa hao wa ujambazi, alikutwa amevaa sare za jeshi hilo, maarufu Jungle Green na kofia aina ya bareti nyeusi ya jeshi hilo pia.

Alisema katika upekuzi huo, pia walikuta redio call, pingu na silaha mbili, zote zikiwa zimefutwa namba zake. Silaha hizo ni Short Gun Pump Action na browning, zote zikiwa na risasi nne kwenye magazine zake.

Kamanda Mambosasa alisema katika uchunguzi wa awali, wamebaini watuhumiwa hao wa ujambazi walifanya matukio ya uhalifu Mkoa wa Pwani, Wilaya ya Mkuranga maeneo ya Vikindu na Kisemvule.

Alidai Jumamosi iliyopita saa mbili usiku watuhumiwa hao walimteka na kumpora Sh. milioni 19.6 mfanyabiashara Salehe Masoud ambaye ni uwakala wa benki na mitandao ya simu.

Kamanda Mambosasa alisema Jeshi la Polisi limejipanga kuhakikisha sikukuu ya Eid El-Hajji inayoadhimishwa leo, inafanyika kwa salama.

## 'Utoaji ajira uzingatie utu wa mwanamke'

**Na Welingtone Masele,**
URAMBO

SERIKALI wilayani Urambo mkoani Tabora imezitaka taasisi, mashirika na kampuni binafsi zinazotoa ajira za muda katika kutekeleza miradi ya kijamii wilayani humo kutoa ajira hizo kwa kuzingatia sifa, haki na utu wa mwanamke.

Hayo yamebainishwa na Ofisa Utamaduni wa halmashauri ya wilaya hiyo, Tito Lulandala, ambaye ni Mratibu wa Kamati ya Wilaya ya kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto, katika semina maalumu ya uwezeshaji kaya maskini iliyofanyika wilayani humo.

Alisema wamebaini kuwa baadhi ya watoa ajira wamekuwa na tabia ya kuajiri watu wasio na sifa huku wengine wakitoa ajira hizo pasipo kuzingatia haki na utu kwa wanamke.

Alisikitishwa na tabia ya baadhi ya watoa ajira kutozingatia hali ya afya za watumishi wao wakiwamo wajawazito kwa kuwachanganya na wenzao katika kazi zozote za kijamii zinazotekelezwa.

Lulandala alisisitiza kuwa ajira yoyote ile inayotolewa kwa jamii iwe ya muda mfupi au mrefu waajiri wanapaswa kuzingatia hali ya waajiriwa wao mfano wajawazito au wenye ulemavu na kutowanyanyapaa.

"Urambo ni moja ya wilaya zinazotekeleza miradi ya kijamii ambazo hutoa ajira za muda kwa wanawake na wanaume ikiwamo za ujenzi wa miundombinu, lakini baadhi ya waajiri hawazingatii hali wala utu kwa waajiriwa wao," alisema.

Alisema wataendelea kufuatilia na kuchukua hatua stahiki dhidi ya waajiri wote wanaoajiri watoto wadogo na wanaowafanyia ukatili wanawake, huku akiitaka jamii kutoa taarifa za siri wanapoona vitendo vya ukiukwaji haki na ukatili kwa wanawake na watoto.

Alitaja baadhi ya kata zilizoko katika wilaya hiyo ambazo matukio ya namna hiyo yamekuwa yakiripotiwa kuwa ni pamoja na Usoke, Ugala, Kiloleni na Usisya.

Naye Mwezeshaji wa Mpango wa Taifa wa kunusuru kaya maskini (TASAF), Deocles Leopold, alisema kuwa awamu ya pili ya mpango huo itatoa ajira za muda mfupi kwa walengwa na watazingatia vigezo vyote vya utoaji ajira.

Alitaja baadhi ya vigezo hivyo kuwa ni mtu mwenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea, mwenye uwezo wa kufanya kazi, mwenye afya njema na ajira hizo zitatolewa bila kubagua jinsia ya mtu.

# Marekani: Mkapa alijitoa huduma za afya Tanzania

**Na Romana Mallya**

UBALOZI wa Marekani nchini, umesema Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, alijitoa kwa dhati kuimarisha mifumo ya utoaji huduma za afya ili kuboresha maisha ya Watanzania.

Kwa mujibu wa taarifa ya Naibu Balozi, Amy Vrampas, iliyotolewa juzi kuhusu kifo cha Mkapa kilichotokea usiku wa kuamkia Ijumaa ya wiki iliyopita, Mkapa, akiwa mwanafunzi, mwanadiplomasia, Waziri wa Mambo ya Nje na Rais, alikuwa rafiki na mshirika wa dhati wa Marekani.

"Ushirika huo uliendelea hata baada ya kumaliza kipindi cha utawala wake, aliendelea kujitoa kwa dhati," Ubalozi wa Marekani ulisema katika taarifa yake hiyo. Vrampas alisema kwa niaba ya Marekani, anawasilisha salamu za rambirambi za dhati kwa watu na serikali kwa kuondokewa na Mzee Mkapa.

Alisema Mzee Mkapa alijitoa maisha yake kuhudumia nchi yake, akifafanua: "Akiwa Rais wa kwanza aliyechaguliwa chini ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi, Mkapa aliendeleza kazi kubwa iliyofanywa na watangulizi wake, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, kwa kuongoza mageuzi makubwa yaliyopelekea Tanzania katika uchumi huru wa soko na kuwa nguzo thabiti ya utulivu katika kanda."

Alisema wanaungana na familia ya Mpaka na Watanzania wote katika kuomboleza msiba huo.

"Tunatafakari na kukumbuka tukiwa na wingi wa shukrani, mchango wake adhimu kwa mafanikio na maendeleo ya Tanzania na ya kanda nzima kwa upana wake," Vrampas alisema katika taarifa yake hiyo.



Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, akiendesha moja ya pikipiki alizokabidhi kwa wakurugenzi wa halmashauri 18 wa Tanzania Bara kupitia mradi wa kudhibiti sumukuvu (TANIPAC), jijini Dodoma, jana. **PICHA: AUGUSTA NJOJI**

# Asilimia 70 ya dhahabu yatoroshwa kinyemela

**Na Happy Severine,** SIMIYU

ASILIMIA 70 ya dhahabu inayochimbwa kwenye machimbo ya Gasuma, Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, hutoroshwa kinyemela na baadhi ya wanunuzi, hali inayodaiwa kuukosesha mkoa huo mapato yatokanayo na madini hayo.

Hayo yameelezwa jana na Ofisa Madini mkoani hapa, Chacha Megewa, kwa Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga, wakati wa ziara yake ya kujionea shughuli za uchimbaji, juzi.

Alisema Idara ya Madini hupokea asilimia 30 pekee ya dhahabu inayouzwa mkoani hapa, huku madini mengi yakitoroshwa kwenda kuuzwa nje ya Simiyu.

"Nilishawaeleza wananchi hawa, ukiwa na madini yako na unaona bei ya hapa (Simiyu) haikuridhishi, njoo tukupe kibali ili ukauze nje ya mkoa wetu.

"Lakini, wananchi hawa ni wakaidi. Hawana ushirikiano kabisa," alisema.

Utoroshaji huo alisema unafifisha mapato ya serikali mkoani hapa na kuwaomba wachimbaji na wanunuzi kutii sheria kwa kuuza mali hiyo katika soko mkoani hapa.

Alisema Idara ya Madini imeamua kutenga eneo kwa ajili ya kujenga ofisi za wanunuzi wa dhahabu mgodini hapo, na tayari ujenzi wake umeshaanza rasmi.

Baadhi ya wachimbaji na wanunuzi wa dhahabu katika mgodi huo wa Gasuma, walisema utoroshwaji huo unatokana na kudhorota kwa bei ya madini mkoani hapa.

Kwa mujibu wa wafanyabiashara hao, bei ya dhahabu katika Mkoa wa Simiyu ni ndogo, ikilinganishwa na masoko ya Mwanza, Mara na Geita.

"Tunaiomba serikali itulinde, soko lipo chini kwa hapa...kule Mwanza na Musoma bei ni nzuri," alisema Cheyo Lugatu, mfanyabiashara wa dhahabu Gasuma.

Dawa Maduhu, alisema wakati wanapokuwa na madini hawaoni wanunuzi, hivyo wanashindwa kujua watoe taarifa wapi.

"Tunamshukuru sana pia Rais John Magufuli ametuongezea thamani ya madini tofauti ilivyokuwa zamani.

"Sasa hivi gramu moja tunauza bei ya juu," Maduhu alisisitiza huku wachimbaji na wanunuzi wengi wakilalamikia anguko la soko la madini mkoani Simiyu."

Kufuatia hali hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga, alitoa onyo kwa watoroshaji madini katika eneo hilo kuwa atakayekamatwa atafunguliwa kesi ya uhujumu uchumi.

Alisema ripoti aliyonayo inaeleza dhahabu inayopatikana mgodini hapo ni chini ya kilo mbili, lakini anafahamu kila siku eneo hilo hutoa zaidi ya kilo mbili na nusu.

Alipiga marufuku wachenjuaji madini eneo hilo wasiokuwa na vibali vya serikali kwa mujibu wa sheria, huku akiwataka wanunuzi wote kuwa na vitambulisho ili kuwatambua kirahisi.

## Hospitali yapata chumba cha maiti

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

HOSPITALI ya Misheni ya Kibara, Bunda mkoani Mara imejengewa chumba cha kuhifadhia maiti na kuwekewa jokofu, hivyo kuondokana na changamoto iliyokuwa ikiikabili.

Hatua hiyo imetokana na wadau mbalimbali wa maendeleo kujitoa kwa kufanya harambee na kuchangia fedha ambazo zimewezesha ujenzi huo.

Chumba hicho kilikabidhiwa juzi mbele ya Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mwanza, Renatus Nkwande, ambaye pia ni Askofu Mlezi wa Kitume katika jimbo la Bunda katika hafla fupi iliyofanyika katika viwanja vya hospitali hiyo.

Katika hafla hiyo ya kukabidhi chumba hicho, Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili, alikuwa mgeni rasimi akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima.

Wadau hao wakiwamo mzawa wa kijiji cha Kibara, Amon Manyama, ambaye pia ni Mratibu wa Miradi kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na mwanasheria Sadock Magai, mzaliwa wa kijiji cha Bunere, walifanya harambee hiyo jijini Dar es salaam mwaka jana na kuchangia fedha taslimu kwa ajili ya nyumba hiyo.

Katika hafla hiyo mwanasheria Magai alisema kuwa Baba Askofu wa kanisa la Katoliki Jimbo Kuu la Mwanza, ambaye pia ni Askofu na Mlezi wa Kitume katika Jimbo la Bunda Renatus Nkwande, aliwaomba kufanya hivyo na kwamba wadau wote kwa ujuma wamechangia zaidi ya Sh. milioni 222 na vifaa mbalimbali vikiwamo vifaa tiba kwa ajili ya kuboresha hospitali hiyo.

"Baada ya Baba Askofu kutuandikia barua akiomba tufanya harambee, tulimkubalia na tukaifanyia huko Dar es Salaam na kufanikiwa kupata fedha hizo na wengine walitoa ahadi.

"Lakini cha kusikitisha na kushangaza na hili lazima niliseme wazi tulichangiwa na watu mbalimbali wa sehemu nyingine, akiwamo Waziri Mkuu Mstafu, Jaji Joseph Warioba. Lakini wa mkoa wetu hasa wilaya yetu ya Bunda, akiwamo aliyekuwa mbunge wa wa jimbo letu, Kangi Lugola, licha ya kumpelekea barua na kumwona moja kwa moja kwa moja na kumwandikia ujumbe mfupi wa simu, hakujibu na wala kwenye harambee hiyo hakufika sasa kwa kweli hii inashangaza.

"Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na Mheshimiwa Baba Askofu hata katika majina ambayo nimeyasoma hapa kwa watu waliochangia katika harambee hiyo, yamo ya kina Macha. Hapa hujasikia majina kama ya Majige, sijui Mafuru na wengine wengi licha ya kuwapatia mwaliko. Kwa kweli inasikitisha sana watu kutokuchangia kwao kwa huduma kama hii muhimu," alisema Magai.

Aliongeza kuwa hiyo mochwari waliyojenga katika hospitali hiyo wakiwa wazawa wa eneo hilo, ni ya kisasa na ina uwezo wa kutunza miili wanne na kuendelea kwa wakati mmoja.

# Tanzania kinara ujenzi miundombinu ya afya

**Na Mwandishi Wetu,** KAHAMA

TANZANIA imetajwa kuwa moja ya nchi bora Afrika katika ujenzi wa miundombinu ya afya kwa kiwango kikubwa na kwamba hayo ni mafanikio makubwa kwa serikali ya awamu ya tano.

Mkurugenzi wa Kinga wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leornad Subi, aliyasema hayo juzi mjini hapa wakati wa ukaguzi shirikishi na kujionea miundombinu mipya ya afya wilayani hapa.

Alisema lengo la wizara kufanya ukaguzi wa miundombinu hiyo ni kuona huduma zinazotolewa kwa wananchi zinakidhi viwango na ni za uhakika.

Pia alisema lengo la serikali ni kuona kuna ufanisi mkubwa wa huduma zinazotolewa katika miundombinu hiyo ikiwa ni pamoja na kuongeza vifaa tiba vitakavyowawezesha wahudumu wa afya kutoa huduma zenye ubora ili kuimarisha afya za wananchi ikiwamo kupunguza vifo vya kinamama na mtoto.

Dk. Subi ameongeza katika ukaguzi wake kwenye Hospitali ya Mji Kahama, amegundua upungufu wa kiutendaji ikiwamo kutokuwekwa vizuri kumbukumbu kwa kuwa kuna masuala ya msingi ambayo wahudumu wa afya wanapaswa kufanya kama inavyotakiwa. Kutokana na upungufu huo, Dk. Subi ameelekeza wataalamu wa afya kuhakikisha wanafanya ukaguzi wa dawa mara kwa mara na kuwasilisha taarifa ya ukaguzi huo kwa mkurugenzi wa halmashauri ili kukabiliana kwa wakati na upungufu wa vifaa tiba.

Alisema serikali imekuwa ikitumia rasilimali nyingi kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa dawa za kutosha, lakini kumekuwa na upotevu wa dawa unaosababishwa na baadhi ya watumishi wasio waaminifu kwa kutofuata mifumo iliyopo au kuweka taarifa vizuri.

Dk. Subi aliongeza kuwa kimsingi idara yake inaangazia zaidi utoaji elimu ya afya kwa wananchi kwa kuwa ndio msingi wa huduma za kinga nchini akitolea mfano Wilaya ya Kahama kuwa na idadi kubwa ya maambukizi ya UKIMWI.

"Wilaya ya Kahama ina wagonjwa 15,000 wanaotumia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI (ARV). Idadi hii ni kubwa sana lakini tukitoa elimu, idadi hii inaweza kupungua kwa kiasi kikubwa na kuokoa fedha nyingi za serikali zinazotumika kununua ARV," alisema. Pia alisema idara yake inashughulikia masuala ya lishe ikiwamo utoaji elimu kwa umma na kuhoji kuwa kwa nini bado kuna udumavu katika jamii kwa kuwa Tanzania ni nchi inayozalisha chakula cha kutosha.

Licha ya uzalishaji huo, bado kuna tatizo la watoto kuwa na udumavu wa kimo na ule wa akili.



Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya Exim, Shani Kinswaga (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu utendaji wa kifedha wa benki hiyo katika robo ya pili ya mwaka 2020 ambapo faida kabla ya kodi imekua kwa asilimia 35 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka uliopita. Wengine ni Naibu Ofisa Mkuu wa Fedha wa benki hiyo, Issa Hamis (kulia) na Mkuu wa Hazina na Masoko, Arafat Haji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataka mwenyekiti aachie ngazi kisa tuhuma ubadhirifu wa fedha

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MWENYEKITI wa Kijiji cha Hanga Ngadinda wilayani Songea, Alphonce Haule, na wenzake wawili wa vitongoji vya Mjimwema na Mdunduwalo katika kijiji hicho, wametakiwa kuachia ngazi nafasi zao kwa muda ili kupisha uchunguzi wa ubadhirifu wa fedha wanazodaiwa kuwachangisha wakulima na wafugaji bila ofisi ya kijiji kuwa na taarifa.

Uamuzi huo ulichukuliwa juzi na wananchi wa kijiji hicho kwenye mkutano maalumu wa dharura ulioandaliwa kwa ajili ya taarifa za sheria za ardhi pamoja na uhakiki wa wananchi wanaoishi katika mazingira magumu.

Suala hilo liliibuka baada ya ajenda hizo kuzimaliza kutokana na mmoja wa wananchi, Lazaro Mhagama, kudai kuwa katika mkutano wa hadhara uliopita, kulikuwa na tuhuma za ubadhirifu wa fedha za kijiji zinazowahusu wenyeviti hao.

Alisema wenyeviti hao walikuwa wakienda Hanga Ngadinda ya zamani ambako walikuwa wakiwatoza wakulima na wafugaji kati ya Sh. 400,000 na 800,000 kwa kutumia vitabu vya stakabadhi ambavyo ofisi ya serikali ya kijiji haivijui.

Mhagama alisema kutokana na tuhuma hizo zinazomhusu Haule, Eleneus Haule wa Mjimwema na Alexia Haule wa Mdunduwalo, ni vyema wasimamishwe uongozi kwa muda ili kupisha uchunguzi.

"Kuna mwanakijiji mwenzetu alitumwa kwenda Hanga Ngadinda ya zamani ambako alifanikiwa kubaini baadhi ya stakabadhi walizozitumia kukusanyia ushuru viongozi hao, zinahofiwa kuwa ni za kughushi," alisema.

Mchungaji Yohana Njovu wa Kanisa la Anglikana, alisema katika mkutano huo kuwa amesikitishwa na ubadhirifu wa fedha za kijji ambao umekuwa ukifanywa na viongozi waliochaguliwa hivi karibuni katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Alishauri uongozi wa kata ya Gumbiro kuona umuhimu wa kuchukua hatua za haraka za kumwomba mkuu wa wilaya ya Songea kufika kijijini hapo ili kuchukua hatua za haraka kuhusiana na tuhuma zinazowakabili viongozi hao.

Naye Basilisi Nyimbo alisema kuwapo kwa ubadhirifu wa fedha za kijiji zinazotokana na ushuru wa mifugo katika Hanga Ngadinda ya zamani ambako kuna hifadhi ya msitu wa serikali na eneo lililotengwa kwa ajili ya wafugaji na wakulima ni aibu kwa uongozi huo.

Kutokana na hatua hiyo, Mwenyekiti wa Serikali wa Kijiji, Haule alisimama na kueleza kuwa anakubaliana na wazo la kujiweka pembeni katika uongozi wakati wa uchunguzi dhidi ya tuhuma zinazomkabili huku akidai kuwa si za kweli.

# Watakiwa kuacha sherehe za ngoma

**Na Christina Haule,** KILOSA

WATENDAJI wa kata nchini wametakiwa kuwahimiza wazazi kuacha kuwekeza nguvu zaidi katika kufanya sherehe za ngoma za watoto badala yake kufanya shughuli za maendeleo hasa zinazohusu elimu.

Mtendaji wa Kata ya Ulaya wilayani hapa, Juma Kizima, alisema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa kata hiyo baada ya kupata elimu ya ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma (PETS) kutoka taasisi isiyo ya kiserikali ya DIRA chini ya ufadhili wa The Foundation for Civil Society (FCS).

Kizima alisema matukio ya ngoma ambayo hufanywa kwa siku tatu mfululizo, yameanza kushika kasi kwa wakazi wa maeneo hayo na mengine katika kipindi baada ya mavuno. Alisema baadhi ya wazazi wamekuwa wakiwekeza kwa muda mrefu kusherehekea na kusahau masuala ya michango ya shule.

Alisema ushiriki halali wa vikao vya kijiji au shule utasaidia wananchi kujua mengi ikiwamo maendeleo ya shule na kijiji kwa ujumla. "Mzazi kuandaa ngoma ambayo itachukua siku nyingi na sherehe zaidi italeta shida kwa mtoto baadaye kutokana na mzazi kukosa uwajibikaji," alisema.

"Wazazi wasiofuatilia maendeleo ya watoto wao, wako maeneo mengi hata Ulaya. Hata mwanafunzi anatoroka shule mzazi haulizi, hajaenda shule mzazi haulizi. Kesho akipata mimba ndiyo anaanza kuuliza kapataje. Sasa tubadilike wazazi," alisisitiza.

Alisema wazazi wanapaswa kutambua wajibu wao kwa jamii hasa watoto ili kuwezesha kufika kwenye matarajio ya kimaisha.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa DIRA, Erasmo Tullo, aliwataka viongozi wa kata kutumia dhana ya uwazi, uwajibikaji na ushirikishwaji itakayowaweka wananchi jirani, hivyo kuwaondoa hofu hasa kwenye miradi ya maeneo yao na kujenga imani ya pamoja.

Tullo pia aliwataka wananchi kutambua kuwa wanapaswa kujua kuwa wana deni kubwa kwa kutoshiriki vikao vya maendeleo au vya shule kwa kuwa wanakosa fursa za ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali zao.

# RPC ataka wapiga ramli wakamatwe

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Debora Magiligimba, ametaka waganga wa kienyeji wanaopiga ramli chonganishi wakamatwe na kuswekwa ndani ikiwa ni hatua ya kutokomeza mauaji ya wazee yatokanayo na imani za kishirikina.

Alisema hayo juzi kwenye mkutano wa Shirika la TAWLAE linalotetea haki za wazee mkoani Shinyanga.

Mkutano huo ulihusisha wakuu wa wilaya za Busega, Magu, Bukombe, Shinyanga, na wakuu wa Polisi kutoka wilaya hizo ukiwa na lengo la kujadili namna ya kutatua changamoto za wazee, yakiwamo mauaji.

Alisema mkoa wa Shinyanga umepunguza mauaji dhidi ya wazee yatokanayo na imani za kishirikina na moja ya mbinu zilizotumika ni kuwakamata waganga wote wa kienyeji ambao wamekuwa wakipiga ramli chonganishi na kuwachukulia hatua kali za kisheria.

"Tumefanikiwa kupunguza mauaji ya wazee yatokanayo na imani za kishirikina baada ya kuwakamata waganga wote wanaopiga ramli chonganishi. Hii ilikuwa chanzo cha mauaji ya wazee ndani ya mkoa," alisema.

"Mfano takwimu za mwaka jana kuanzia Januari hadi Juni, zinaonyesha kuwa mkoa wetu wa Shinyanga waliuawa wazee saba, mmoja kutokana na imani za kishirikina na sita kwa sababu zingine zikiwamo za migogoro ya mali. Lakini mwaka huu, kuanzia Januari hadi Juni, ameuawa mzee mmoja tu," aliongeza.

Nao wenyeviti wa mabaraza ya wazee kutoka wilaya hizo, wakisoma taarifa za wazee kwa nyakati tofauti, walibainisha changamoto ambazo bado zinawakabili ikiwamo ukosefu wa vitambulisho vya matibabu, uhaba dawa kwa wazee, kutelekezewa wajukuu na mauaji.

Mratibu wa TAWLAE, Eliasenya Nnko, alisema wameendesha mkutano huo kwa kushirikisha wilaya za Busega, Magu na Bukombe kwa lengo la kubadilishana uzoefu ili kutatua changamoto zinazowakabili wazee ikiwamo kutokomeza mauaji dhidi yao.

Aidha, aliipongeza serikali pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama nchini kwa kupunguza matukio ya mauaji ya wazee tofauti na miaka ya nyuma, walivyokuwa wakiuawa kutokana na imani za kishirikina hasa wale waliokuwa na macho mekundu.

# TBS yatoa elimu kuhusu sumukuvu

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limetoa elimu ili kujenga uelewa kwa wananchi wa Wilaya za Handeni na Kilindi mkoani Tanga kuhusu sumukuvu, madhara yake na jinsi ya kukabiliana na tatizo hilo.

Akizungumza juzi wakati wa utoaji elimu hiyo, Ofisa Usalama wa Chakula Mkuu wa TBS, Dk. Candida Shirima, alisema elimu hiyo imetolewa kwenye wilaya hizo kwa kuwa ziko kwenye ukanda wenye hali ya hewa inayowezesha ustawi wa fangasi wanaozalisha sumukuvu kwenye mazao ya chakula hususan mahindi na karanga, hivyo ni muhimu wananchi wake wakafahamu jinsi ya kudhibiti sumu hiyo.

Dk. Shirima alisema TBS imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ili kukabiliana na tatizo la sumukuvu kwa lengo la kulinda afya ya jamii na kuwezesha biashara ya mazao ya chakula.

Kwa mujibu wa Dk. Shirima, TBS imechukua hatua hiyo muhimu ya kutoa kipaumbele katika kuelimisha jamii namna ya kukabiliana na sumukuvu hususan katika kipindi hiki cha msimu wa mavuno ya mahindi ili wananchi wafahamu taratibu muhimu zinazopaswa kuzingatiwa ili kukabiliana na sumukuvu katika mnyororo wa mazao kuanzia yanapokuwa shambani na baada ya kuvunwa, wakati wa kukausha, usafirishaji, uhifadhi na uandaaji.

Alisema sumukuvu ni aina ya sumu inayozalishwa na jamii ya fangasi kwenye mazao ya chakula na kwamba mazao yanayoathiriwa zaidi ni nafaka hasa mahindi na mbegu za mafuta hasa karanga.

Sumukuvu, alisema kuzalishwa kwenye mazao yakiwa katika hatua mbalimbali kuanzia shambani na baada ya kuvunwa endapo taratibu bora za kilimo, uvunaji, ukaushaji, usafirishaji, uhifadhi na uandaaji hazitazingatiwa.

Pia alisema mambo yanayowezesha uzalishaji wa sumukuvu ni pamoja na uwapo wa jamii ya fangasi husika na kuchochewa na hali ya hewa ya joto kali na unyevu, ukame na wadudu waharibifu.

Wataalamu wa TBS, alisema wametoa elimu ya sumukuvu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na wananchi wengine kwa ujumla katika wilaya za Kilindi na Handeni kupitia kwenye shule, masoko, minada, mikutano ya vijiji, magulio, kliniki za mama na mtoto na maeneo mengine ya biashara.

Alisema kupitia elimu iliyotolewa, jamii ilielimishwa pia kuhusu madhara ya kiafya yatokanayo na sumukuvu ambayo hujitokeza ndani ya muda mfupi ikiwa ni pamoja na maumivu ya tumbo, kuathirika kwa ini na hata kifo endapo mtu atakula kiwango kikubwa cha sumukuvu ambacho mwili hautaweza kukihimili.

Pia alisema sumukuvu inaweza pia kusababisha madhara yanayotokea baada ya muda mrefu ambayo ni pamoja na saratani ya ini, upungufu wa kinga mwilini na udumavu.

Kuhusu namna ya kudhibiti sumukuvu kwenye mazao, Dk. Shirima alihimiza hatua muhimu zichukuliwe kabla na baada ya kuvuna mazao.

Alitaja hatua hizo kuwa ni pamoja na kupanda kwa wakati mbegu zilizothibitishwa na taasisi za udhibiti wa viwango vya ubora wa mbegu, kuhakikisha shamba ni safi wakati wote, kutumia viuatilifu mara wanapoona dalili za visumbufu (wadudu, magonjwa) kwenye mazao, kuvuna kwa wakati na kuondoa mazao shambani baada ya kuvuna.



Mkurugenzi wa Vodacom Tanzania Foundation, Rosalynn Mworia (wa pili kushoto), akikabidhi moja ya mashine kwa ajili ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati (Njiti) kwa Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili (wa tatu kulia), kwa ajili ya Hospitali ya St. Mary's iliyopo Kibara, wilaya humo jana. Wengine ni Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mwanza, Renatus Nkwande na Mganga Mkuu wa hospitali hiyo, Dk. Samuel Paul. Vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. 57,881,360 vilivyotolewa na taasisi hiyo, kusaidia watoto kupumua, kuongeza joto na kuwapa tiba mwanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC ahamishia ofisi chini ya mti

**Na Steven William,** MUHEZA

MKUU wa Wilaya ya Muheza, Mhandisi Mwanasha Tumbo, amehamishia ofisi chini ya mti katika kiwanja cha wazi ili kusikiliza kero za wananchi na kwamba atafanya hivyo kila Jumatano.

Tumbo amesema ameamua kufanya hivyo kutokana na watu wenye kero kuwa wengi, hivyo kuzidiwa na kwamba muda mwingine hufika mpaka saa nne usiku kusikiliza matatizo ya wananchi.

Akizungumza juzi mjini hapa, mkuu huyo wa wilaya alisema wananchi wa Muheza wana kero nyingi, hivyo kufika ofisini kwake kuziwasilisha ili kuzipatia ufumbuzi. Alisema wananchi wanapofika asubuhi anasikiliza kero za kila mmoja kwa kuwaita majina au vikundi na kuzitolea uamuzi na zingine kuzielekeza kwa wakuu wa idara husika katika halmashauri.

Tumbo alisema hatua hiyo imesababisha wananchi kujazana ofisini kwake, hivyo ameamua kufanya Jumatano ya kila wiki kuwa siku maalum ya kusikiliza kero za wananchi.


Mkuu huyo wa wilaya alifafanua kuwa kusikiliza kero na kuzitafutia ufumbuzi ni moja ya majukumu yake aliyotumwa na Rais John Magufuli kuyatekeleza.

Mbali na kero za wananchi, alisema ametenga Jumanne ya kila wiki kusikiliza kero za watumishi ndani ya wilaya ili kuhakikisha kunakuwa na ufanisi katika utendaji wa kazi katika utumishi wa umma.

Katika kufanya hivyo, pia amekuwa akitatua kero za wafanyakazi wanaokuwa na migogoro na waajiri wao, huku akiwashirikisha maofisa wa kazi kutoka mkoani na taifa.

Kutokana na hatua hiyo, baadhi ya wananchi wamempongeza kiongozi huyo kwa kuwajali na kusikiliza matatizo yao.

Mmoja wa wananchi, Abdallah Shekalao, alisema kiongozi huyo ni mfano wa kuigwa na kwamba viongozi na watendaji wote wangekuwa wanafanya hivyo, migogoro mingi ingetatuliwa katika ngazi za chini na kumalizika kabisa.



Ukurasa 13

Haya sasa njooni tujitathmini


Ukurasa 14

## Mhadhiri awafumbua macho namna kutojua soko kunawaachia kinamama 'majanga'


# BUFE

IJUMAA JULAI 31, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




# Biashara ya mchanga unaochimbwa ilivyo mgogoro sugu Mkuranga

Shughuli ya kuchimba mchanga Mkuranga ikiendelea. **PICHA: MAKTABA**

**Na Yasmine Protace,**
Mkuranga

SEKTA ya mchanga ina mapato na ajira kubwa kwa wakazi wa Wilaya ya Mkuranga, mkoa wa Pwani na ina mchango mkubwa, inayowezesha mapato kuendelea kupatikana.

Msisitizo unaoelekezwa hapo, ni hitaji la maendeleo yanayaopaswa kuendelea kupatikana katika hali inayoendana na kuwepo usimamizi mzuri wa rasilimali hiyo.

Hivi karibuni wachimba mchanga wilayani Mkuranga, mkoa wa Pwani, walikutana na Mkuu wa Wilaya, Filbeto Sanga, kuwasilisha madai kuhusu athari za upande wao katika jukumu la uchimbaji mchanga,

Katika mkutano huo ulioandaliwa na Ofisi ya Wilaya Mkuranga, wadau hao wachimbaji na wauzaji mchanga walitoa malalamiko yao kwa Mkuu wa Wilaya, ikiwamo kusimamishwa jukumu lao.

Said Salum, ni msafirishaji mchanga anasema, kunapokuwapo usimamishaji idadi ya magari au kupunguzwa kiwango cha kuchimba mchanga umekuwa na athari kwao wachimbaji.

Analalamika awali walinunua mchanga kila lori kwa Sh. 40,000, lakini baadaye ilipanda, akifafanua:"Cha kushangaza bei imepanda kutoka kiasi cha Sh. elfu sitini hadi sitini na tano."

Salum anasema kutokana na ongezeko la bei, waliona ni bora wakasimamisha kuchukua mchanga na wameegesha magari yao.

Pia, anasema hivi sasa wanakumbana na kikwazo kikubwa kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), alilalamilika kutokana na anachokitamka 'kuwavizia' wanapotoka Mkuranga katika mashimo, wakiwataka waeleze wanakoenda kuuza mchanga, ili wawapatie risiti walazoenda kuwauzia watu mchanga.

"Mtu hujauza mchanga, risiti inatoka wapi?" anahoji Abdallah Ally, mmiliki wa shimo la mchanga huku akiongeza kuwa sura nyingine ya kero iko katika ubovu wa barabara, hali inayochangia gharama za ziada.

Ally Magenge, kutoka Ofisi ya Mazingira Mkoa wa Dar es Salaam, anasema wamekuwa wakipata malalamiko kutoka kwa wananchi wanaodai wachimbaji mchanga, wanawaharibia mazingira, nyumba nyingi zimeharibiwa na uchimbaji mchanga.

Katibu wa Wachimba Mchanga hao wa Mkuranga, Mbaraka Madenge, anasema kupandishwa bei ya mchanga, kumetokana na mashamba kupandishwa bei.

Pia, mbali naye kuilalamikia TRA kutokana na hilo alilolitaja, anawataka wahusika wa mazingira kutoa elimu ili nao wawasaidie wadau wa mchanga kufikwa na elimu ya mlipa kodi.

Mkuu wa Wilaya Mkuranga, Filbeto Sanga, anasema biashara ya mchanga ina mapato na ajira kwa wakazi wa wilaya yake, akifafanua wadau wa mchanga wanapaswa kulitazama, kupitia uendeshaji wake kwa ufanisi.

Sanga anasema, falsafa yake ni kuiona wilaya inaendelea kupata maendeleo, ikiwamo kupatikana ajira kutoka maeneo mbalimbali ya nchi.

"Ujenzi wa Dar es Salaam, sehemu kubwa unategemea mchanga kutoka Mkuranga," anasema Sanga, akiongeza mkakati uliopo ni wa Polisi kuweka utaratibu utakaohakikisha wasafirishaji mchanga wawe madereva walio na sifa stahiki.

Suala la uchimbaji mchanga na athari zake imekuwa la kujirudia kila wakati ikiwa na historia zake, mathalan mwaka 2017, katika kikoa cha Baraza la Madiwani, ikiibuka hoja iliyoungwa mkono na serikali ya wilaya, pia madiwani kuhusiana na hifadhi ya mazingira.

UCHUMI

# Kijiji kilichojitunuku kwa staili Utawala Bora kijinufaishe kwa uchumi maliasili

## • Hifadhi misitu, mavuno yake kujenga kijiji • Hujuma za wafugaji, wakulima bado shida

**Na Beatrice Philemon, aliyekuwa TUNDURU**

MIAKA 15 na ushee iliyopita, Tunduru ilikuwa wilaya ya mafichoni mkoani Ruvuma na penye hali duni kimaendeleo. Leo hii ikirejeshwa tamko hilo, mtu anapaswa kutafakari mara kadhaa ukweli huo, maana kuna kila sababu ya kuguna, ile kuwa historia. Mkombozi nani?... Barabara ya lami!

Hapo ndiko kunapatikana kijiji cha Mindu, umbali wa maili 40 (kilomita 24.86), kutoka mjini Tunduru akiwa na wasifu wa kubarikiwa utajiri wa misitu ya asili, katika Msitu wa Hifadhi uliogeuka mzizi wa mapato kwa ajili ya maendeleo ya wanakijiji.

Pia, shambani kuna mazao ya biashara kama ufuta, choroko, mbaazi na korosho, vyote vikiwafanikishia kupata zahanati, shule ya msingi na sekondari .

Ni namna gani juhudi za kujiongeza zinafanyika mahali hapo kugeuza utajiri huo kuwa mali ya asili? Darasa linaanzia katika mafunzo ya utawala bora kijijini, ambayo sasa yanawaletea mabadiliko makubwa kiuchumi na kijamii na manufaa kujumuishwa hata kwa Halmashauri ya Wilaya Tunduru.



Katibu wa Maliasili ya Kijiji cha Mindu, Angelelus Macha, akiongea na wajumbe wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji cha Mindu, kuhusu uharibifu wa msitu wa Liwina kutokana na wafugaji. **PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON**

### KATIBU KIJIJI

Mwandishi wa Nipashe aliyezuru kijijini hapo hivi karibuni alikutana na Katibu wa Maliasili ya Kijiji cha Mindu, Angelelus Macha, anayetamka: "Bila utawala bora, kijiji hakiwezi kutumia rasilimali za misitu au fedha za kijiji kwa faida ya umma, vinginevyo kutakuwa na ubadhirifu."

Anasema, mafunzo ya utawala bora waliopata kutoka Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), umewafanikisha kutumia vyema rasilimali msitu yao.

Kutokana na matumizi mazuri ya fedha , hivi sasa wamefanikiwa kujenga ghala la kuhifadhi mazao ambalo hivi sasa limeanza kutumiwa na vyama vya ushirika vya msingi vya mazao (AMCOS), wanaovuna mazao na kupitia ghala lao, kijiji kinapata fedha kutokana na ushuru wa kuhifadhi mazao.

Mpango ulioko hivi sasa ni kwamba wanajenga shule ya sekondari ya kata, ambayo tayari ina vyumba vitano vya madarasa, ofisi moja na matundu sita ya choo.

Msitu wa Hifadhi ya Kijiji Liwina, kilichoko katika ndani ya kijiji Mindu kilichoanzishwa mwaka 1974 katika zama za 'operesheni vijiji' nchini, kina jumla ya wanavjiji 1867 una hekta 3,713 ya misitu ya asili.

> **Mifugo ipo mingi sana inaharibu vyanzo vya maji, nyasi hakuna zinakauka, hakuna amani kwenye msitu wetu, kwa sababu wanakata miti kwa ajili ya makazi ya mifugo yao.**

Macha anasema kuwepo uwazi kwenye mapato yanayotokana na mazao ya misitu na vyanzo vingine vya kijiji, taarifa zake za mapato na matumizi, husomewa wanakijiji kila baada ya miezi mitatu, kupitia Mkutano Mkuu wa Kijiji kwa wananchi.

"Sisi kama kijiji tuna vyanzo vingi vya mapato ikiwamo ushuru wa minara ya simu, ruzuku kutoka halmashauri na faini zinazotozwa kwa wafugaji wanaoingiza mifugo ndani ya msitu wa hifadhi ya kijiji kwa ajili ya malisho na makazi," anasema Macha.

Anaeleza, wamefanikiwa katika suala la usimamizi na hifadhi misitu, ila bado wanakwama katika mikasa ya ng'ombe wanaoingizwa msituni, wakilalama faini na wanazotozwa wafugaji na baadhi ya matukio kupotosha haki ya kijiji.

Malalamiko yake ni kwamba hivi sasa wanavijiji wa Mindu, Namakambale na Songambele wanafanya kazi katika mazingira magumu, wakidai mifugo inaingizwa msituni na baadaye wamiliki kutozwa faini.

### MIKASA

"Mwaka 2018 tulikamata wafugaji wawili kutoka kijiji cha mindu wakilisha mifugo ndani ya Msitu wa Hifadhi ya Kijiji unaoitwa Liwina 'Forest Reserve' kinyume cha sheria," anasema



Ofisa Mtendaji wa Kijiji, Mohamed Said, akionyesha ghala lililojengwa na kijiji cha Mindu, kwa ajili ya kuhifadhi mazao.

Macha anasimulia tukio la mfugaji wa kwanza, alikamatwa na ng'ombe 200 na alipopelekwa katika Kituo cha Polisi jirani alitakiwa kulipa faini ya Sh. milioni mbili baadaye alitoroka.

Anataja mfugaji mwingine, pia alinaswa na ng'ombe 300 katika Msitu wa Liwina na anasimulia: "Tulimkamata mfugaji huyu tukiwa kwenye doria katika msitu wetu wa hifadhi.

"Tulikuwa tunafanya doria ili kukamata wavamizi au waharifu wanaovamia msitu kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji wa ng'ombe, malisho na utengenezaji wa mbao."

Kwa mujibu wa Macha, viongozi wa kijiji wamehangaika kufuatilia malipo katika mamlaka za kisheria, pasipo mafanikio, hali inayofanya kijiji kutofanikiwa na malipo, ambayo ni sehemu ya mapato wanayotarajia kusaidia kujenga shule ya sekondari.

"Tunataka (mfugaji) akamatwe tena, kwa sababu mwaka jana mwezi wa 12 tulikutana naye na kumuuliza faini yetu atalipa lini?

"Akasema tayari ameishalipa Sh. 500,000 kwa... Sisi kama wanakijiji hatuna uhakika na anachosema kwa sababu mpaka sasa hakuna hela yoyote iliyolipwa serikali ya kijiji," anasema.

Rai yao wananchi hivi sasa ni kusaidiwa katika madai hayo anayodai inawafanyisha kazi ya uhifadhi na usimamizi wa misitu katika mazingira magumu.

"Kwanza hatupati posho na fedha tunayoipata kutokana na faini zinazotozwa kwa wafugaji, zinatumika katika maendeleo ya kijiji, masuala ya uhifadhi wa misitu na kufanya doria," anasema Macha.

Hivi sasa viongozi wa kijiji wanasema wameandika barua kuhusu suala hilo na kuipeleka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru tangu Juni 15 mwaka huu, yenye nakala kwa Mkuu wa Wilaya na ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ili wawasaidie kwa hatua stahiki ichukuliwe dhidi ya suala hilo.

### MTENDAJI KIJIJI

Ofisa Mtendaji wa Kijiji, Mohamed Said, anasema msitu wa Liwina unaharibiwa na wafugaji kutokana na ubishi wao katika ulipaji faini.

"Tunaomba serikali ifuatilie ambaye amesababisha kijiji kupata hasara, kwa sababu hata Ofisa Misitu, pia hakuwa na ushirikiano mzuri kwenye ufuatiliaji wa suala hili," anasema Saidi.

Anataja manufaa waliofaidika na utawala bora kijijini hapo, mwaka 2017 kijiji kiliuza mbao zenye thamani ya Sh. milioni 5.2 na kutumia fedha hizo kujenga ghala la kuhifadhia mazao na fedha zilizobaki walitumia kuhifadhi misitu.

Anaorodesha manufaa ambayo ni kujengwa madarasa matano, ofisi moja ya walimu, matundu sita ya vyoo na hadi sasa bado wanahitaji vyumba vitatu vya madarasa na ofisi ya walimu kuwawezeshea mazingira mazuri ya kusoma, yatakayowasaidia kupata matokeo mazuri.

"Shule hii ni mpya, imeanza ujenzi mwaka 2019 na itakuwa na uwezo wa kuchukua zaidi ya wanafunzi 800 hadi 1000, kuanzia 'form one hadi four'..." anasema.

### WAJUMBE MALIASILI

Mjumbe wa kamati ya Maliasili ya Kijiji cha Mindu, Edmund Komba, anasema uhifadhi wa msitu unawanufaisha na kuwepo mvua ya kila mara, inayowanufaisha katika kilimo na ustawi misitu.

"Watu wakivamia msitu na kuharibu, sisi hatunufaiki chochote. Kwa, mfano kama huyo aliyechukua hela yetu hiyo, ni rushwa, anatukatisha tamaa katika uhifadhi wa misitu. Ushauri wetu serikali itusimamie twende bega kwa bega ili tupate hela yetu ya kijiji," anasema.

Komba hivi sasa uongozi wa kijiji unahangaika kupata Sh. milioni tatu kutoka kwa mfugaji ndiyo maana wanakijiji wanaomba serikali iingilie kati, ili wapate Sh. milioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari ya kata na miradi mingine ya kijiji.

Christina Zuberi, ni Mjumbe wa Kamati ya Maliasili Kijiji cha Mindu, anasema Msitu wa Liwina wameshavuna mara moja tu na kupata hela na tayari wameshanufaika.

"Kutokana na usimamizi wa msitu tulifanya doria kwa watu waliokuwa wanavuna mbao, tulishika mbao tukaziuza na kupata fedha za kujenga ghala," anasema.

Anasema watu wanachoma moto msituni, wanalisha mifugo ndani ya msitu na ndio ya vyanzo vya maji, ombi letu tusaidiwe kusimamia msitu yetu.

Hamza Mohamed, Mjumbe wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji Mindu, anasema huwa wanafanya doria msituni na wastani wa mara kadhaa kila mwezi .

"Mifugo ipo mingi sana inaharibu vyanzo vya maji, nyasi hakuna zinakauka, hakuna amani kwenye msitu wetu, kwa sababu wanakata miti kwa ajili ya makazi ya mifugo yao," anasena na kuongeza:

"Hivi sasa kuna eneo kubwa la msitu ambalo limeishaharibiwa na wafugaji na hatujui wanatoka wapi."

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Augustino Andrea, anasema wafugaji wameharibu mazingira ya msitu unaonaza kutoweka kutokana na uvamizi kilimo.

"Viongozi wetu wanakuja, kinachopatikana wanachukua wanaenda kutengeneza kwao, wanajinufaisha wenyewe," anasema.

Klio chake ni ugumu katika ufanyaji doria, kwani hawana fedha za kuwalipa wajumbe wanaofanya doria.

### OFISA TARAFA

Nipashe ilizungumza na Ofisa Misitu Tarafa, Stanley Balueshi, anayekana dai la wafugaji walikamatwa msituni kumataifa fedha akitamka 'ni uongo.'


"Sijachukua hela yoyote kutoka kwa mfugaji, kwanza mimi ndiye niliyemkamata mfugaji akiwa anapitisha ng'ombe kutoka kijiji cha Mkowela kwenda kijiji cha Tinginya, nikiwa na watu wa Shirika la Mpingo. Tulikuwa tunatoka kijiji cha Ng'apa kwa ajili ya shughuli zetu kiofisi," anasema.

Anasema baada ya kumkata walimpeleka Kijiji cha Mindu kumsajili na kisjha mchakato wa kisheria ulichukua mkondo wake kisheria.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Haya sasa njooni tujitathmini






**NA JOSEPH KULANGWA**

NINA kijukuu, kina miaka mitatu tu hivi. Kipenda sifa sana tu. Kikinunuliwa ki-nguo kipya au hata cha mtumba, kitazunguka vyumba vyote vya wapangaji wenzetu kutafuta kuambiwa umependeza. Kitafurahi sana kikisifiwa.

Lakini, sikilaumu sana kwa sababu binadamu ndivyo tulivyoumbwa, ingawa hiki kwa kuzingatia umri kimezidi. Ukikiambia hujapendeza, kinakununia kana kwamba kinakulisha. Lakini. Kwa huruma ukibadilisha msimamo kinafurahi tu na kinarejesha urafiki.

Ndivyo tulivyo. Inawezekana kimerithi kwangu babu mtu, sijaambiwa lakini inawezekana mimi zamani nilitaka kusifiwa hivyo,ingawa kijijini tuliko kuwa enzi hizo hatukuwa na mitumba, hata nguo tulizovaa wengine tulirithi kwa kaka au dada zetu.

Saa ngapi usifiwe kwa kupewa jishati reefu la kaka yakolililomruka, na kwako kuwa kama kanzu.

Lakini. Ilikuwa safi tu, kwa sababu shati hilo uliweza kulivaa bila nguo nyingine ndani, naamanisha kaptula au bukta, kwa sababu hakukuwa na nguo za ndani enzi hizo hata kwa watu wazima. Mnashangaa nini sasa? Kila mwenye umri wangu arudi nyuma kwenye historia yake.

Tuache hayo. Rais John Magufuli akalivunja Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Juni 16 jijini Dodoma. Bungelikapigwa kufuli memba waliokuwamo wakafunguliwa lango kuu kurudi walikotoka wakaanze upya kama wanataka kurejea. Ingawa aliwaombea kurudi hasa aliowaita wavaa nguo za kijani. wale wengine walijiombea kimya kimya.

Inanikumbusha, nikiwa sekondari, aliwahi kututonya Mkuu wa Shule dhidi ya vurugu na ukosefu wa nidhamu shuleni, kwamba ukikosea siku tunakufukuza unaondoka mwenyewe na sanduku lako kama ulivyokuja.

Wabunge wameondoka, kila mtu kivyake kurudi kwao kuitafuta ridhaa. Kimbembe hicho. Mtu unajitafakari ulifanya nini miaka yote mitano mjengoni! Ulichangia nini ukiwa bungeni kwa maslahi ya wapiga kura wako? Si kutafuta kusifiwa tu kama mjukuu wangu!

Je, ulitimiza uliyowaahidi mpaka wakakuchagua? Kama jibu ni ndiyo, heriyako. Lakini, kama siyo, tafuta pengine pa kutokea, kwa sababu ujasiriamali upo na kitambulisho ni Sh. 20,000 kwa mwaka.

Wapiga kura nanyi ni wakati sasa wa kuwaangalia hao mliowapeleka bungeni, je walikidhi kile mlichowatuma kufanya? Au waliambulia kuitwa waheshimiwa tu na kupigiwa makofi ya mezani na kumulikwa na makamera ya video na magazeti, ili wapitevyumba vya wapangaji kutafuta umependeza?

Lakini umma waWatanzania nao utakaa na kujiuliza, je, kweli bado ni muda mwafaka kwa vigezo vya kuchaguliwa wabunge kuendelea kuwa hivyo hivyo, vikiwamo vya kujua kusoma na kuandika tu?

Tufikiriejamani wakati wetu huu. Tujiulize je, kilichofanya mikutano ya Bunge isiwe mubashara bado kipo na kina uzito au la? Tutafakari basi?

Je, ni kweli kwamba kama Bunge lingeonyeshwa mbashara, tusingejenga reli ya kisasa, tusingejenga barabara za juu, tusingejenga mitambo ya kuzalisha umeme ya Julius Nyerere, tusingehamia Dodoma? Tujiulize!

Je, ni kweli kwamba kwa kutoonyesha Bunge mbashara, zile chokochoko za waheshimiwa zilifunikwa? Aah! Mbona zilikuwapo jamani, hasa jamaa walipoamua kuikimbia corona bungeni na kwenda kupiga nyungu kwa siku 14. Vijembe kwa sana tu.

Pale jamaa alipovunjika mfupa wa mguu, vijembe kwa kwenda mbele, eti waheshimiwa wa zamani Msukuma unasemaje, Silinde je? Lijualikali? Tena hapo bajeti ya serikali inajadiliwa, lakini vijembe kama kawa, tena wakati mwingine vikianzia kitini, wacha wee!

Msidhani hayakuonekana haya, vilipu kibao vipo kwenye mitandao ya kijamii. Havifichi kitu hata kidogo. Sasa hivyo ndivyo tutavitumia sisi wapiga kura, kufanya tathmini na kuona nini kifanyike.

Haitoshi kuuliza maswali na kutuletea pesa za Mfuko wa Jimbo kwa ajili ya barabara na maji, pia kuangalia staha, hulka na kaliba ya mtakaokuwa mnatuwakilisha tena katika miaka mingine mitanoi jayo. Tutakuwa makini sana, ili nchi hii ifike tunakotaka, hutakiwa na haki pia ya kukufuatilia ni ile mbashara.

Mtaji wenu wabumbe ni macho na masikio yetu. Kwa hiyo, mtakapotuahidi tena mtuahidi tabia njema bungeni na Bunge Mbashara! Alamsiki.

**Simu: (+255) 0713 410008 na baruapepe: jkulangwa@yahoo.com**

BIASHARA

KINAMAMA WALIPOINGIZWA DARASANI...

# Mhadhiri awafumbua macho namna kutojua soko kunawaachia 'majanga'

• Wakiri 'zinadoda' ugenini, nchini • Waonyeshwa njia tatu za kufanikiwa



Mkufunzi Mariam Tambwe (kushoto), akiendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wanawake wanaofanya biashara nje ya mipaka ya nchi. **PICHA: SABATO KASIKA**

**Na Sabato Kasika**

KATIKA shughuli za biashara kuna mbinu mbalimbali wafanyabiashara wanazitumia kufikia malengo yao.

Lakini, baadhi ya wanaojishughulisha na biashara kuvuka wanafanya shughuli hizo kwa mazoea, hali inayochangia kukwama.

Ni mambo yanayojiri kutoka kwa jumla ya wanawake 40 wa mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Mara na Kigoma, waliofundishwa mbinu muhimu za kuwawezesha kufanikiwa katika biashara zao.

Mafunzo hayo ya siku tano kwa wanawake wanaofanya biashara nje ya mipaka ya Tanzania, yaliandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), chini ya Mkufunzi Mariam Tambwe,

Mkufunzi huyo, ambaye pia ni Mhadhiri wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), anaainisha biashara kuwa na mbinu nyingi, lakini hizo tatu ndizo muhimu kwa ajili kufikia malengo stahiki.

Anataja muhimu kwa mfanyabiashara ni kuwa na chapa; kufanya utafiti wa soko kabla ya kuanza biashara; na umuhimu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama), kwa kuwa dunia sasa imekuwa kijiji.

> **"Kwa majibu wa Mamlaka ya Mawasiliano nchini, asilimia 25 ya Watanzania, wanatumia mitandao ya kijamii kama jukwaa la kuwaunganisha katika shughuli zao mbalimbali.**

### WAFANYABIASHARA

Upendo Nkwira, kutoka Manyovu Kigoma, ni mama anayefanya biashara ya kuingia nchini Burundi kwa miaka miwili sasa, ananunua na kuuza matunda katika nchi jirani ya Burundi.

Pia, anaeleza 'majanga yake' ya anaponunua na kuuza katika nchi hiyo, lakini bado mambo hayajamuendea vizuri, akifafanua:"Biashara zangu zimekuwa zikiniozea na kupata hasara kwa kukosa wateja. Kwa mfano, ninaweza kununua machungwa ya shilingi laki mbili na kupata nusu ya pesa niliyonunua, kwa sababu wateja ni wachache kule."

Upendo anasema alianza kukata tamaa, lakini sasa anaendelea kujipanga upya, baada ya kupigwa msasa wa siku tano wa jinsi ya kufanya biashara ya kupata faida badala ya hasara.

Mwemzake Mariam Makoko, kutoka Tanga, anasema biashara ndani ya mipaka ya Tanzania ina matatizo yanayochangia kukwamisha hatua za maendeleo ya wanajamii.

### UTAFITI

Kama ilivyo kwa hoja ya Rais mjenzi wa taifa kubwa kibiashara duniani China, Mao Tse Tung, pasipo utafiti 'hakuna haki ya kunena jambo'naye mhadhiri huyo ana hoja kama hiyo kutoka katika nadharia ya masoko.

Anasema, ni muhimu kwa mtu anapotaka kufanya biashara, la kwanza kwake liangukie utafiti wa masoko, ili kubaini aina ya biashara anapaswa kuifanya na idadi ya wateja walioko kama wanakidhi matakwa yake, kabla hajajitosa tu.

"Watu wengi wanafanya biashara kienyeji. Anaamka na kuanza kukaanga vitumbua bila ya kujua labda wateja wanataka mihogo, matokeo yake vitumbua vinakosa soko," anasema Mariam.

Pia, anafafanua kuna wakati mtu anaweza kujibebesha dhana ya uchawi kwenye biashara, kumbe inaangukia mtazamo wa kisayansi na ukweli wa mambo, ikianzia mwenyewe hakufanya utafiti wa soko, kabla ya kuamua kufanya aina ya biashara isiyo na wateja.

"Kwenu mnaofanya biashara nje ya mipaka ya Tanzania, mnatakiwa kuwa makini sana, kwani unaweza kubeba mzigo mkubwa kwenda Kenya na kujikuta hunakosa soko, huku umetumia gharama kubwa," anasema.

Mariam anahimiza suala la utafiti ni muhimu zaidi kwa kwa kila mfanyabiashara, ili kujua ni bidhaa au vitu gani vinavyohitajika sokoni.

### CHAPA BIASHARA

Mariam anaeleza kwa mfano, iwapo mtu anauza viatu, ni lazima awe na chapa yake itakayomtambulisha na umarufu wake, ili aweze kupata wateja wengi zaidi.

"Hata ukiwa na biashara ya kawaida tu, chapa yako inaweza kukufanya ukawa maarufu kwa watu na siyo vibaya ukajiita mama viatu ili ujulikane kwa jina hilo na hiyo inakuwa ni chapa yako ya biashara," anasema.

Anarejea mfano wake wa kuwapo watu wengi wanaouza viatu, nguo na vingine, na ili kujitofautisha nao sokoni, ni muhimu ubunifu utumike kumpa muizaji wateja wengi katika biashara.

### KWANINI TEHEMA?

Anasema, ukuaji wa tekonolojia habari na mawasiliano umewezesha mengi, ikiwamo urahisishaji wa ununuzi kupitia mtandao mbalimbali kama ya simu za mkononi.

"Unaweza kuona bidhaa kabla ya kuinunua, hivyo tumieni Tehama kutangaza biashara zenu na siyo kuuza sura kama ambavyo baadhi ya wanawake wamekuwa wakifanya," anasema.

Aidha anasema, kupitia teknolojia ya mawasiliano wanaweza kupata elimu ya biashara kwa kujifunza mengi yahusuyo biashara kupitia tovuti, blogi na mitandao ya kijamii kama 'facebook.'

"Katika teknolojia ya mawasiliano, kuna utoaji wa huduma bora kwa wateja, kuwapo kwa uhusiano wa karibu kati ya mzalishaji na mfanyabiashara, msambazaji na mteja," anasema.

### OFISA TGNP

Ofisa Programu Msaidizi wa TGNP, Jackson Malangalila, anasema katika karne iliyoko, Tehama haikwepeki, hivyo kinachotakiwa ni kila mwanamke kwenda na wakati.

"Kwa majibu wa Mamlaka ya Mawasiliano nchini, asilimia 25 ya Watanzania, wanatumia mitandao ya kijamii kama jukwaa la kuwaunganisha katika shughuli zao mbalimbali, " anasema Malangalila.

Anafafanua kuwa mitandao ya kijamii pia inatumiwa na wafanyabiashara kubadilishana mawazo, uzoefu na mengine muhimu kwa ajili ya maendeleo ya shughuli zao za kila siku.

"Sisi TGNP, tupo tayari kuwafundisha wafanyabiashara jinsi ya kufungua barua pepe na namna ya kutumia mitandao ya kijamii kwa ajili ya biashara, ili waweze kuwasiliana na wengine wa ndani na nje ya nchi," anasema.



# Serikali kudhibiti sumukuvu kwenye mazao

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

SERIKALI imejipanga kupambana na tatizo la sumukuvu kwenye mazao ya wakulima nchini kwa kutoa Dola za Marekani milioni 35.3 kwa ajili ya mapambano hayo.

Hayo yalibainishwa jana na Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alipokuwa akikabidhi pikipiki kwa wakurugenzi wa halmashauri 18 wa Tanzania Bara kwa kupitia Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu (TANIPAC).

Alisema utafiti unaonyesha mazao ya karanga na mahindi ndio yanayoshambuliwa zaidi na sumukuvu hapa nchini. Kusaya alisema kuwa sumukuvu inatokana na kutofuatwa kwa hatua sahihi kwenye upatikanaji wa mbegu, upandaji, upaliliaji, uvunaji na wakati wa kuhifadhi mazao hayo baada ya mavuno.

"Hivyo serikali kulinda usalama wa wananchi wake tumepanga kujenga maabara kuu ya mazao itakayokuwa inaangalia ubora wa mazao yote yatakayokuwa yanazalishwa hapa nchini ili kuimarisha usalama wa mazao na vilevile kulinda uchumi wa taifa pamoja na maisha ya Watanzania kwa ujumla," alisema.

Alisema mkakati wa serikali pia katika kukabiliana na tatizo hilo, kitajengwa kituo cha umahiri wilayani Kongwa kitakachokuwa ni sehemu muhimu katika sekta ya kilimo kwa kutoa taaluma mbalimbali za kilimo.

Pia alisema kupitia Mradi wa TANIPAC, halmashauri 12 zitajengewa maghala 12 na mawili visiwani Zanzibar ili kusaidia wakulima kuhifadhi mazao yao.

Kusaya alisema kuwa serikali kupitia wataalamu wake wataendelea kutoa elimu kwa Watanzania ili kupata uelewa kwa jamii juu ya kuhifadhi mazao yao kwa ufasaha.

Naye, Mwakilishi wa Katibu Mkuu TAMISEMI, Mkurugenzi wa Sekta za Uchumi na Uzalishaji wa TAMISEMI, Leo Martin, alisema wakurugenzi katika mamlaka za serikali za mitaa wamekabidhiwa pikipiki hizo kama vitendea kazi vya kuwafikia wananchi kwenye maeneo yao.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Itilima, alishauri kuwapo kwa ushirikiano wa karibu katika vita dhidi ya sumukuvu nchini ili kufikia malengo ya kuwa na usalama wa mazao yanayozalishwa.



Mchuuzi wa miwa akiandaa bidhaa yake kando ya barabara jijini Dodoma jana, bila kuchukua tahadhari ya vumbi kitendo ambacho ni hatari kwa afya ya walaji. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# H'shauri yatenga mil. 500/- ujenzi kituo wajasiriamali

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetenga kiasi cha Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo maalum cha kuwasaidia wajasiriamali wadogo.

Mkuu wa kitego cha vijana na maendeleo ya jamii wa Jiji hilo, Sharifa Nabalang'anya, aliiambia Nipashe ofisini kwake.

Alisema kituo hicho kitajengwa eneo la Nzuguni jijini hapa na lina ukubwa wa hekari nane.

"Halmashauri yetu imetenga kiasi cha Sh. milioni 500 kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali kujenga mabanda ya kuuza bidhaa zao pamoja na kuwasaidia kuwatafutia masoko ya bidhaa hizo," alisema.

Pia, idara yake pamoja na kuwasaidia mikopo makundi ya vijana, kinamama na wenye ulemavu ina jukumu la kutoa elimu kwa wahusika ili kukuza mitaji yao.

Alitaja makundi ya wajasiriamali hao watakaopewa eneo hilo kuwa wazalishaji na watengenezaji wa bidhaa mbalimbali za ngozi na mafundi ushonaji.

Aliyataja makundi mengine kuwa ni wauzaji na wazalishaji wa bidhaa za vyakula, matunda, pamoja na watengenezaji wa bidhaa za urembo wa asili.

Aliongeza kundi lingine kuwa ni wafugaji wa kuku wa mayai na nyama pamoja na wafugaji wa ng'ombe wa maziwa na nyama.

Kadhalika, alisema kwa wajasiriamali wa bidhaa ya ng'ombe wanatarajia kuweka kituo maalum cha kukusanya bidhaa za maziwa ili kuwarahisishia wateja kuwapata eneo moja.

Halmashauri pia imejiandaa kuwasaidia wajasiriamali hao kuzalisha bidhaa bora ambazo zimeboreshwa kwa viwango vilivyowekwa na kupendekezwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Vile vile, wameandaa utaratibu maalum wa kuwasaidia wajasiriamali husika kupata mikopo ya mitaji kwa kuwaunganisha na taasisi mbalimbali za fedha.

Pia alisema lengo la halmashauri hiyo ni kuwajengea uwezo wajasiriamali hao ili kuweza kuhudumia wateja waliongezeka kutokana na serikali kuhamishia makao makuu Dodoma.

# Shirika lasaidia sekondari 22 vifaa kunawia mikono

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Compassion Tanzania, limetoa vifaa vya kunawia mikono vyenye thamani ya Sh. milioni 10, kwa shule za sekondari 22, zilizopo pembezoni mwa Jiji la Dodoma ili kuendelea kuchukua tahadhari za kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona pamoja na magonjwa ya mlipuko.

Akipokea msaada huo, Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Watoto kutoka Wizara ya Maendeleo ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwajuma Magwiza, alisema msaada huo utasaidia kuendeleza hali ya usafi kwa wanafunzi katika shule hizo.

Alisema kuwa chimbuko la msaada huo ni serikali kuomba wadau mbalimbali nchini kusaidia vifaa hivyo baada ya Rais John Magufuli, kutangaza kufunguliwa kwa shule.

"Kutokana na kuwapo kwa ugonjwa wa corona wakati ule wa kilele cha Siku ya Mtoto wa Afrika, tuliamua kuomba wadau mbalimbali, watusaidie kupata vifaa hivi vya kunawia mikono kutokana na wakati ule shule zilikuwa zinakwenda kufunguliwa," alifafanua Magwiza.

Pia alisema kutokana na msaada huo, wanafunzi wataendelea kujilinda na maambukizi ya corona wakati wote watakapokuwa katika mazingira ya shule.

Vile vile alisema kuwa vifaa hivyo vitasaidia wanafunzi kuendeleza usafi ili kuepukana na magonjwa ya mlipuko ikiwamo kuhara damu.

"Suala la usafi ni lazima sio tu kwa ajili ya kujilinda na corona, lakini kimsingi usafi unatakiwa kila wakati na kwa msaada huu sasa tutaweza kuwalinda watoto wetu na magonjwa mengine ya mlipuko ambayo pia ni hatari kwa afya zao," alibainisha.

Alitoa wito kwa wadau wengine kuendelea kujitolea kusaidia katika maeneo mengine ili kuwezesha watoto kusoma katika mazingira rafiki na salama.

Alisema pia kuna upungufu katika maeneo ya shule, ikiwamo ukosefu wa huduma ya maji pamoja na matundu ya vyoo ya kutosheleza mahitaji.

Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano kwa Umma kutoka Compassion, Melkizedeck Karol, alisema kuwa msaada huo ni mwendelezo wa jitihada zao katika kusaidia jamii zinazoishi katika mazingira magumu.

Karol, alisema kuwa mpaka sasa wameshasaidia jamii katika masula ya kujikinga na corona na kiasi cha Sh. bilioni 1.2 kimetumika katika halmashauri 14, nchini.

"Katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika tumetumia Sh. milioni 100, lakini katika halmashauri 14, nchini toka kuanza jitihada za kusaidia jamii kwenye janga la corona, tumetumia kiasi cha Sh. bilioni 1.2 mpaka sasa," alisema Karol.

Naye Kaimu Ofisa Elimu Sekondari wa Jiji la Dodoma, Ferdinand Komba, alisema msaada huo umekuja wakati muafaka hasa kwa shule zilizopo pembezoni.

"Kunawa mikono kumesaidia hadi hii leo hakuna mwanafunzi hata mmoja ambaye ameripotiwa kuwa na virusi vya corona, lakini hata magonjwa mlipuko kama vile kuhara damu yamepungua kwa kiasi kikubwa sana," alisema Komba.



# Wanafunzi vyuo vikuu wafundwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAFUNZI wanaojiandaa kujiunga na vyuo vikuu nchini wametakiwa kuchagua fani wanazozipenda kwa lengo la kupata ujuzi na umahiri utakaowawezesha kuhimili ushindani kwenye soko la ajira.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, wakati akifungua mafunzo ya siku moja kuhusu namna ya kuomba mikopo kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) kwa vijana wanaojiandaa kujiunga na elimu ya juu mwaka huu.

Chalamila alisema ipo dhana ya vijana wengi kukimbilia fani ya ualimu wakiamini kuwa huko ndiko kwenye uhakika wa wao kupata ajira, jambo ambalo kwa sasa si sahihi.

"Vijana wengi wanashawishika kwenda kusoma fani ya ualimu hata kama hawaipendi wakiamini kuwa kwenye ualimu ndiko kuna uhakika wa ajira. Hili kwa sasa si sahihi, hivyo nawashauri kwamba chagueni fani mnazozipenda ili msome kwa moyo mmoja na ndipo mtapata ujuzi na kuwa mahiri kiasi cha kumudu ushindani kwenye soko la ajira," alisema Chalamila.

Alisema ajira serikalini zipo, lakini zinapotolewa vijana wengi wanakosa sifa kutokana na aina ya masomo waliyosoma ambayo hayaendani na nafasi za ajira zinazotolewa.

"Ukiangalia mitaani vijana waliohitimu ni wengi, lakini serikali ikitoa nafasi za ajira hasa za kitaaluma unakuta tunaanza kuwahesabu. Kwa mfano zikitolewa nafasi za walimu wa sayansi, unakuta tunaanza kuwahesabu vijana maana wahitimu wengi walio mitaani ni walimu wa masomo ya sanaa," alisema Chalamila.

Alisema ili vijana wawe na uhakika wa ajira, ni vizuri wakasoma fani wanazozipenda ambako watasoma kwa bidii na kuwa na ujuzi ambao hata wakiingia kwenye ushindani wanashinda na kupata ajira bila wasiwasi.

Maofisa wa HELSB walisema wameamua kutoa elimu kwa waombaji wa mikopo ili waelewe namna sahihi ya kuomba mikopo hiyo na kuepuka kukosea na hivyo kukosa vigezo vya kukopeshwa.

Mkuu wa Mawasiliano wa HELSB, Omega Ngole, alisema vijana wengi wanashindwa kupata mikopo kwa kushindwa kujaza fomu za maombi kwa usahihi jambo ambalo mwaka huu wasingependa lijitokeze.

Ngole aliwataka waombaji wote kusoma na kuzingatia miongozo inayotolewa na HELSB ili wasikosee na kusababisha washindwe kupata mkopo.

# TAKUKURU yaokoa mil. 406.6/-

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, imeokoa zaidi ya Sh. milioni 406.6 ambazo zilikuwa zimetumiwa vibaya na baadhi ya viongozi.

Fedha hizo zilitumiwa na viongozi wa vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS), vyama vya akiba vya kuweka na kukopa (SACCOS), halmashauri na taasisi mbalimbali zinazokusanya mapato ya serikali.

Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Abdaudi Mbura, alisema hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya robo tatu ya mwaka kuanzia Aprili mpaka Juni. Alisema taasisi hiyo ilifuatilia fedha hizo katika halmashauri zote za mkoa huo.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. milioni 205.3 ziliokolewa kutoka kwa watumishi waliokuwa wamepewa jukumu la kukusanya mapato ya serikali kwa kutumia mashine za kielektroniki (POS) ambazo baada ya kukusanya hawakuziwasilisha serikalini.

Mbura alisema Sh. milioni 10 ziliokolewa kutoka kwa diwani aliyemaliza muda wake katika Wilaya ya Chunya ambaye hakulitaja jina lake na kwamba alipewa fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Amos Makala.

Diwani huyo, alisema baada ya kupewa fedha hizo, hakujenga vyumba vya madarasa na badala yake alizichukua na kuzifanya kuwa mali yake binafsi lakini baada ya kufuatilia na kubaini kuwa amezihodhi, walimfuatilia na akazirejesha.

Vilevile alisema Sh. milioni 177.1 ziliokolewa kutoka katika vyama vya ushirika ambazo zilikuwa zimetafunwa na baadhi ya viongozi wa vyama hivyo na baadhi ya wanachama na watu lakini hawakuzirejesha.

"Lakini Sh. milioni 6.8 ziliokolewa kutoka kwenye vikundi ambavyo vilikuwa vimekopeshwa na halmashauri kutoka katika fungu la asilimia 10 la mapato ya ndani. Vikundi hivi huwa vikikopeshwa vinatakiwa kurejesha na huwa vinapangiwa muda, lakini havikurejesha," alisema Mbura.

Pia alisema Sh. milioni 6.1 ziliokolewa kutoka katika sekta ya ujenzi, mabaraza ya kata, ardhi na binafsi na kwamba zilikuwa hazijawasilishwa katika mamlaka husika ikiwamo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Katika hatua nyingine, Mbura alisema katika kipindi hicho cha miezi mitatu, taasisi hiyo ilipokea taarifa 137 za tuhuma za rushwa na makosa mengine.

Alisema kati ya taarifa hizo, 29 zilikuwa zinazihusu halmashauri mbalimbali, wafanyabiashara taarifa 19, mashirika ya umma (11), mahakama (12), ardhi (12), vyama vya ushirika (tisa) na maliasili moja.

"Lakini katika kipindi hicho tuliendelea na kesi 16 ambapo tulishinda nne, tulishindwa moja na zingine zinaendelea katika hatua mbalimbali na tulifungua kesi mpya tano," alisema Mbura.

Pia alisisitiza kuwa katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye uchaguzi mkuu, taasisi hiyo itaendelea na utoaji wa elimu kwa jamii kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu vitendo vya rushwa.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, akiwahutubia washiriki wa mafunzo ya udadisi wa sensa ya kilimo, mifugo na uvuvi katika mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Songwe na Rukwa, yaliyoandaliwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) jijini Mbeya hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Lukuvi mgeni rasmi ufunguzi Nanenane

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye ufunguzi wa Maonyesho ya Wakulima (Nanenane) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yanayotarajiwa kuanza kesho.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, alisema jana wakati wa kikao cha mwisho cha maandalizi ambacho kilifanyika katika katika uwanja wa John Mwakangale jijini hapa, ambao unatumika kwa ajili ya maonyesho hayo.

Kasesela ambaye alikuwa mwenyekiti wa kikao hicho, alisema katika kikao cha awali sekretarieti ya maandalizi iliagizwa kuwaandikia viongozi mbalimbali wa kitaifa kuwaomba wawe wageni rasmi kwenye maonyesho hayo.

Alisema kabla ya kikao hicho, walipokea barua za viongozi hao kukubali mwaliko huo, hivyo akawataka viongozi wa halmashauri zote za mikoa ya kanda hiyo kujiandaa kwa ajili ya kuwapokea wageni hao.

"Tunatarajia maonyesho haya yatafungwa Agosti 8 na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ambaye tulimwomba na alikubali kuja kutufungia. Sasa tuendelee na maandalizi ya vipando na kila taasisi inatakiwa kujiandaa vizuri ili maonyesho yetu yawe na uhalisia," alisema Kasesela.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mapokezi ya Maonyesho hayo, alisema maandalizi yanaendelea na hivyo kila atakayehudhuria atahudumiwa vizuri.


Ntinika alisema maonyesho ya mwaka huu yatakuwa bora kuliko miaka yote kwa maelezo kuwa kwa sasa wameboresha miundombinu ya barabara kwenye uwanja huo na hivyo hakutakuwa na vumbi kama ambavyo imekuwa ikitokea miaka mingine.

Alisisitiza kuwa kwa mwaka huu wameshaweka utaratibu mzuri wa upatikanaji wa washindi wa maonyesho na hivyo kila halmashauri na taasisi zitakazohudhuria zitakuwa na nafasi.

"Tuwahakikishie wageni wetu wote kuwa Jiji la Mbeya liko salama na mimi ndiyo Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hii, hivyo tutahakikisha kila mmoja anakuwa salama," alisema Ntinika.

Katika hatua nyingine, Kasesela aliuagiza uongozi wa benki ya NMB kuongeza fedha kwa ajili ya maonyesho hayo kwa maelezo kuwa mchango ambao benki hiyo imetoa ni kidogo.

Vilevile alisema watahakikisha wanaboresha maonyesho hayo kila mwaka ili wananchi wajifunze zaidi kuhusu kilimo na kukuza uchumi wa wananchi.



# NEC yasisitiza maofisa uchaguzi kuzijua sheria

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAOFISA uchaguzi na wasaidizi wamesisitizwa kusoma kanuni na sheria za uchaguzi, pamoja na maelekezo ili kuwaongoza kutoa mafunzo kwa watendaji watakaotumika katika mchakato wa uchaguzi.

Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Tanzania (NEC), Jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Mbarouk Salim Mbarouk, alisema hayo wakati akifunga mafunzo kwa maofisa hao katika ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdulwakil, Kikwajuni. Alisema, uchaguzi utakaofanyika baadaye mwaka huu, unatarajiwa kuwa huru na haki, hivyo watendaji hao wana wajibu wa kuzingatia majukumu yao na kuwasimamia kikamilifu walio chini yao. "Pamoja na uzoefu mlionao ni nyenzo muhimu katika kufanikisha uchaguzi, uzoefu wenu pia unaweza kumponza mtu kwa kufikiri unajua kila kitu na kujisahau kusoma uliofundishwa," alisema.

Alisema jukumu lililopo mbele yao ni kuteua na kutoa mafunzo kwa watendaji wa vituo katika wilaya zao kwa lengo la kuona uchaguzi unamalizika bila ya matatizo yoyote.

Mbarouk, alisema Tume inaamini kuwateua wao na kuwandaa kuwa wakufunzi katika mafunzo ya watendaji wa uchaguzi ngazi ya vituo wakiwa na imani kwamba kazi hiyo wataifanya kwa ufanisi na kuwezesha uchaguzi huo kufanyika kwa mafanikio makubwa.

"Ni vyema kutumia mbinu, ujuzi na elimu ya ufundishaji mlioipata ili kuhakikisha ujumbe uliopo katika mada mtakazowasilisha unawafikia walengwa," alisema.

Hata hivyo, alisema changamoto zilizojadiliwa katika mafunzo hayo ikiwamo suala la muda zitiliwe msisitizo wakati wa kuendesha mafunzo kwa watendaji hao ili kufikia lengo lililokusudiwa.

Kwa upande wake, Khamis Ngwali Makame, Msimamizi Msaidizi Jimbo la Tumbatu, alisema kupitia mafunzo hayo amejifunza kwamba uchaguzi wa mwaka huu unatakiwa kuwa wazi na mifumo ambayo iliyoandaliwa itakuwa inarekodi moja kwa moja matokeo na uteuzi wa wagombea vitu ambavyo mwanzo vilikuwa vinafanywa siri kuonyeshwa.

Riziki Khamis Yahya ni ofisa msimamizi msaidizi wa uchaguzi Jimbo la Mwera, alisema atahakikisha anayasimamia yote aliyofundishwa ili kuona uchaguzi unakwenda katika ustawi unaotakiwa.

"Tunaamini wakufunzi wetu walitufundisha kwa mujibu wa Katiba, kanuni na sheria nasi tuhakikisha tunatumia mafunzo haya kuyafikisha na kuwakilisha vizuri taifa letu kwa usahihi na uzalendo," alisema.

Kwa upande wake Hawa Seif Amour, ambaye ni msaidizi msimamizi wa uchaguzi Jimbo la Mfenesini, aliihakikishia Tume kusimamia uchaguzi na kuendesha kwa amani na utulivu.




Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Hamid Mahmoud akizindua shughuli za uchaguzi mkuu mjini Zanzibar jana, utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu. Kulia ni Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi, Thabit Idarous Faina. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri ataka utunzaji siri Taasisi ya Elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, ameitaka Bodi ya Ushauri ya Taasisi ya Elimu Zanzibar kuhakikisha inaendelea kutunza siri za kazi zao ili amani na utulivu uendelee kuimarika katika taasisi zao.

Akizungumza wakati akivunja bodi iliyomaliza muda wake na kuizindua bodi mpya ya taasisi hiyo, alisema ni lazima kuhakikisha wanalinda dhamana walizopewa kwa kufuata sheria na kanuni zilizopo.

Aliwataka kushirikiana vyema kuimarisha Taasisi ya Elimu, kwa kubuni njia mbadala zikazowezesha kukua zaidi.

Wajumbe wa bodi hiyo na wafanyakazi wa taasisi hiyo pia wametakiwa kuweka uzalendo mbele katika nchi na kutochanganya masuala ya kazi na siasa ambayo yanaweza kuiharibu kazi yao.

Alisema hivi sasa ni wakati wa uchaguzi, hivyo ni vyema kuwa makini wakati wa kampeni unapofika, kwa kutoacha kazi na kujikita kwenye siasa na kwamba kwa anayehitaji kufanya hivyo afuate utaratibu ili kila upande usiweze kuharibikiwa.

Aliipongeza bodi iliyomaliza muda wake kwa mafanikio makubwa iliyoyapata katika kuhakikisha kazi za taasisi hiyo zinakwenda vizuri kwa kuwawekea mazingira mazuri ya utendaji wa kazi zao, ana imani kuwa kurejeshwa kwao tena katika bodi hiyo wataendeleza mazuri zaidi.

Mwenyekiti aliyemaliza muda wake na kurudishwa tena katika bodi hiyo, Dk. Abdullah Ismail Kanduru, alisema haikuwa rahisi kufanya kazi yao kwa pamoja kutokana na ujuzi wa kila mjumbe wa bodi, lakini anashukuru kutokana na hekima na busara za wajumbe na uelewa wameshirikiana na kukubali kukosoana na hatimaye kupata mafanikio mazuri.

Aliahidi kuendeleza jitihada hizo na kurekebisha kasoro walizoziacha ili waweze kufikia malengo yaliyowekwa na taasisi hiyo.

Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Mwalimu Suleiman Yahya alisema imepata mafanikio mengi ikiwamo kupatiwa ofisi ili kupunguza ufinyu wa nafasi pamoja na kuongezewa bajeti.

Aliishukuru Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa jitihada inazozichukua kuhakikisha imepata hati miliki ya eneo la wizara ambalo wanatarajia kujenga jengo jengine jipya muda mfupi ujao.

Bodi mpya ya Taasisi ya Elimu Zanzibar imeundwa ikiwa na wajumbe wanane chini ya Mwenyekiti wake Dk. Abdullah Ismail kanduru, ambayo itadumu kwa miaka 100.

# Corona ilivyoathiri ajira sekta binafsi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema zaidi ya wafanyakazi 5,000 katika sekta binafsi ikiwamo hoteli za kitalii wameathirika na ugonjwa wa corona huku wengine wakipoteza ajira.

Waziri wa kazi uwezeshaji wanawake, wazee na watoto Maudline Castico, alisema hayo wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, huku akiwataka waajiri sekta binafsi ambao wamewapa likizo bila ya malipo wafanyakazi wao kuwafikiria na kuwapatia fedha za kujikimu maisha.

Alisema serikali inalifahamu tatizo hilo ambalo limewapata wafanyakazi wengi katika sekta binafsi ikiwamo ya utalii huku hoteli nyingi zikiendelea kufungwa kutokana na janga hilo kuendelea kuleta maafa duniani.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inaendelea na mchakato wa kufanya tathmini kuhusu wafanyakazi wa sekta mbalimbali ambao wameathirika na ugonjwa wa corona... tunawaomba waajiri wa sekta ya utalii kuwafikiria wafanyakazi waliopewa likizo bila ya malipo ili waweze kujikimu," alisema.

Baadhi ya asasi za kiraia zimeiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwasaidia wafanyakazi wa sekta ya utalii pamoja na makundi mengine ya wajasiriamali ili waweze kukabiliana na athari za ugonjwa wa corona ambazo zimewafanya kushindwa kufanya biashara zao.

Mkurugenzi wa asasi ya kiraia inayoshughulikia Vijana Zanzibar Youth Forum (ZYF), Maulid Suleiman, alisema sekta ya utalii imeathirika na ugonjwa wa corona na vijana waliowekeza katika sekta hiyo ikiwamo wasambazaji wa vyakula hotelini na watembezaji wa wageni wamepoteza ajira kwa zaidi ya miezi minne sasa.

Alisema licha ya serikali kuruhusu kuanza tena kwa sekta ya utalii kwa kuingia kwa wageni nchini, bado hali haijawa nzuri kutokana na ukweli wenyewe kwamba huko Ulaya ugonjwa wa corona bado upo ukisababisha maafa makubwa.

"Taasisi ya Vijana Zanzibar Youth Forum, imesikitishwa na hali ya kuzorota kwa sekta ya utalii ambayo imeathirika kutokana na ugonjwa wa corona... tunaiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwasaidia wafanyabiashara wazalendo wanaotoa huduma katika hoteli za kitalii ambazo zimeathirika," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


**IN THE DISTRICT COURT OF ILALA**
**.................................................................**
**AT SAMORA AVENUE**

**MISC CIVIL APPEAL CASE, MATR CAUSE/REV, PROB ADMIN, CAUSE NO. -----------2019**

**JOYCE FRANCIS OKWIDIBA PLAINIFF/APPELANT**
**VERSUS**
**LETSHEGO BANK (T) LTD......DEFENDANT/RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE MENTION/HEARING**

THE NOTICE that the above case has been fixed for mention/Hearing on 12th day of August 2020at 8.30Morning Before Hon OBASI SR/M/RM
YOU ARE required to appear in this court without fail and you must produce to that day all the documents upon which you intended to reply in support your case
Given Under my hand and Seal of the court this 29th Day of July 2020

**RESIDENT MAGISTRATE**

**COPY TO BE SERVED UPON**
**DANIEL RABIEL MUSHI**
**0767 826 311**
**DAR ES SALAAM**

115837801

---

**IN THE DISTRICT COURT OF MKURANGA**
**AT MKURANGA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 6 OF 2020**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**YOHANA PAULO MURUTA**
**AND IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR THE LETTER OF ADMINISTRATION BY SESILIA YOHANA PAULO**

**GENERAL CITATION**

A person claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 17 day of August 2020.

Given under my hand and seal of the court this 17 day of July 2020

RESIDENT MAGISTRATE
17/07/2020

115838402

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Sepratus K. Byarushengo** amepoteza kadi ya gari aina ya Fuso namba **T 331 BBM** ambayo iliungua kwenye kiwanda cha kahawa huko Karagwe. Taarifa zipo kituo cha Polisi Bukoba
**KAG/BUK/RB/565969/2020.**

115838502

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI.

**Justine Severin Tibalinda** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki aina ya **TVS** yenye namba ya Usajili namba **MC574 CLC** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**KJN/IR/672/2020**

115837002

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI.

**Bernadeta Aggrey Msongole** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA VITS** yenye namba ya Usajili namba **T976 DRS** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**KW/RB/3846/2020**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA KINONDONI**
**SHAURI LA MIRATHI NAMBA. 52 YA 2020**
**ELIAH JULIUS IDEJE........................MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**JULIUS PETER IDEJE........................MAREHEMU**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Kwa kuwa mwombaji ameleta maombi ambayo maelezo ya maombi yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hii, kwa hiyo mtu yeyote mwenye maslahi katika maombi ya mwombaji tajwa hapo juu anapaswa kuweka pingamizi na kuhudhuria katika mahakama hii ya Wilaya binafsi au wakili au mwakilishi ambaye anayeruhusiwa kabla ya siku ya tarehe 17 mwezi 08, 2020, mbele ya Mheshimiwa MWAKALINGA saa mbili kamili (2:00) asubuhi. Kwa kuwa siku hiyo ni kusikilizwa kwa shauri unatakiwa kuja na vielelezo vyote vinayohusiana na maombi ya mwombaji huyu.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama leo tarehe 27, Mwezi 07 mwaka 2020.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI
DAR ES SALAAM

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ELEONORA MAKISHE LYIMO**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T; 692 BVY** AINA YA NADIA RANGI YA SILVER CHASSIS NAMBA **SNX100050254,** ENGINE NAMBA 4FE67423 AMBAYO IMEPOTEA MWAKA HUU.
KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA ELEONORA MAKISHE LYIMO KWA SIMU NAMBA **0754-541261 AU 0714-193424**
**RB NAMBA SHY/RB/2020,**
**CONTROL NAMBA 9910818122414.**

115838302

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI.

**FAIZA DAUD YAKUB** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 682 BJB.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi:
Taarifa ya Polisi:
**BUG/RB/551152/2020.**

115838202

---


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

## India yanunua ndege za kivita ikihofia China

**NEW DELH,** India

JESHI la India limepokea ndege tano za kivita aina ya Rafale huku kukiwa na wasiwasi mkubwa kati yake na China.

Ndege hizo ni miongoni mwa makubaliano ya Taifa hilo na lile la Ufaransa yaliofanyika mwaka 2016 kununua ndege 36.Delhi inatumai kuimarisha jeshi lake la angani linalotumia ndege za zamani za kisoviet kupitia ununuzi wa ndege hizo mpya. Lakini watalaamu wanaonya kwamba ndege hizo haziwezi kutumika moja kwa moja iwapo kutakuwa na vita.

Mwanaanga mstaafu, Pranab Barbora, ambaye alisimamia ununuzi wa ndege za kivita aina ya jaguar aliambia BBC kwamba kuwasili kwa Rafale ni hatua nzuri kwasasabu itaimarisha uwezo wa jeshi la angani.

''Lakini itachukua muda kabla ya ndege hizi kufanza kufanya kazi . Lazima uweke msururu wa kimkakati, kuwafunza mafundi na wafanyakazi wa ardini nchini India'', alisema Barbora.

Aliongezea kwamba inachukua hadi miaka miwili kabla ya kikosi kipya kuanza operesheni.

Kikosi hicho cha Rafale kitaanza kufanya kazi kitakapomiliki takriban ndege 18. Kuwasili kwa ndege nyingine kunatarajiwa kukamilika mwakani. Ndege hizo zilizotengenezwa na kampuni ya Ufaransa ya Dassault Aviation, ziliondoka nchini Ufaransa siku ya Jumatatu na kuwasili UAE ambapo zilitua kwa muda kabla ya kuondoka na kuelekea India.

Safari hiyo ilionyesha uwezo wa ndege hizo pamoja na uwezo wa kujazwa mafuta zikiwa angani.

Ndege aina ya Rafale ni ndege ilio na uwezo wa kufanya vitu tofauti ikiwamo kusafiri umbali mkubwa, kufanya mashambulizi ya angani na ardhini bila kukosa.

Wachambuzi wanasema kwamba kuwasili kwa ndege hiyo kutapiga jeki motisha ya jeshi la angani ambalo limekuwa likikabiliwa na upungufu wa ndege za kijeshi. **BBC**

# Zimbabwe yakubali kulipa fidia wakulima wazungu

**HARARE,** Zimbabwe

SERIKALI ya Zimbabwe imesaini makubaliano ya kulipa dola bilioni 3.5 za Kimarekani kama fidia kwa wakulima wazungu ambao ardhi yao ilichukuliwa na aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, marehemu Robert Mugabe.

Rais wa Zimbabwe wa sasa, Emmerson Mnangagwa, alisema uamuzi huo umefanyika kwa mujibu wa katiba ili kufidia wakulima wazungu kwa hatua yao ya kuiboresha ardhi kwa kujenga mabwawa kabla ya ardhi hiyo kuchukuliwa kwa nguvu.

Kiongozi wa muungano wa kibiashara wa wakulima, Andrew Pascoe, ameonyesha kuridhishwa na makubaliano hayo.

Pascoe ambaye muungano wake unajumuisha wakulima walionyang'anywa kwa nguvu ardhi yao katika miaka ya 2000 alisema: "Baada ya karibu miaka 20 ya mzozo kuhusu suala la ardhi, wawakilishi wa wakulima walipoteza ardhi kufuatia mageuzi ya sera za ardhi hatimaye wamekubaliana na wawakilishi wa serikali kumaliza mzozo huo. Kwangu mimi uamuzi huu ni kama miujiza."

**Wakulima wapatao 4,000 walipoteza ardhi yao kufuatia mageuzi yalioanzishwa na Hayati Robert Mugabe, ambayo mara nyingi yalikumbwa na vurugu.**

Makubaliano hayo yanaainisha kuwa asilimia 50 ya dola bilioni 3.5 italipwa katika muda wa miezi 12 huku fedha zilizosalia zikilipwa katika muda wa miaka mitano.

Rais Mnangagwa alisema makubaliano hayo ni ya kihistoria kwani yanaashiria mwanzo mpya katika Taifa hilo la kusini mwa Afrika.

Mnangagwa aliyeingia madarakani mwaka 2017 baada ya Rais Mugabe kulazimishwa kujiuzulu, amekuwa akiwahimiza wakulima wazungu kutuma maombi ya kumiliki baadhi ya vipande vya ardhi ili kuwekeza.

Ofisa mmoja katika muungano huo wa kibiashara wa wakulima alisema zaidi ya wakulima 3,500 wametuma maombi ya kutaka kulipwa fidia.

Kulingana na makubaliano hayo, Zimbabwe itatoa dhamana za muda mrefu na pia itaunda timu inayojumuisha wakulima hao kuomba msaada zaidi kutoka kwa wafadhili wa kimataifa ili kupata fedha za kuwalipa fidia wakulima hao.

Wakulima wapatao 4,000 walipoteza ardhi yao kufuatia mageuzi yalioanzishwa na Hayati Robert Mugabe, ambayo mara nyingi yalikumbwa na vurugu.

Wakulima wa kizungu walikuwa wanamiliki sehemu kubwa ya ardhi yenye rutuba ya kilimo. Hivi sasa ardhi ya kilimo inamilikiwa na serikali. **DW**



Baadhi ya raia wa kigeni nchini Zimbabwe, wakipongeza uamuzi uliochukuliwa na serikali ya nchi hiyo wa kuwalipa fidia baada ya kunyang'anywa mashamba yao. **PICHA: REUTERS**

# Marekani kuondoa wanajeshi 12,000 Ujerumani

**WASHINGTON,** Marekani

SERIKALI ya Marekani imesema itaondoa wanajeshi wake wapatao 12,000 waliopo Ujerumani katika kile kinachoelezwa kama hatua ya kimkakati ya kupanga tena wanajeshi wake Ulaya.

Takriban wanajeshi 6,400 wa Marekani watarejeshwa nyumbani huku wengine wakipelekwa katika nchi zingine ambazo ni washirika wa NATO kama vile Italia na Ubelgiji.

Rais wa Marekani, Donald Trump, alisema hatua hiyo imetokana na Ujerumani kushindwa kufikia malengo ya NATO upande wa pesa za matumizi kwa ajili ya ulinzi.

Lakini suala hilo limepingwa vikali bungeni hasa wale wanaoamini kuwa hatua hiyo itaimarisha Urusi. Maofisa waandamizi wa Ujerumani pia nao wameonesha wasiwasi wao.

"Hatutaki kuendelea kudanganywa, Tunapunguza wanajeshi kwa sababu hawalipii gharama zao," alisema Rais Trump.

Kwa kipindi kirefu, Rais Trump amekuwa akilalamika kwamba washirika wa NATO wa Ulaya wanastahili kuongeza kiwango chao cha matumizi kwa ajili ya ulinzi wao wenyewe.

Aliongeza kuwa washirika hao hawastahili kuitegemea Marekani kuchukua mzigo mkubwa zaidi wa gharama za kuendeleza muungano huo.

Majadiliano kati ya washirika wa muungano huo yanazingatia kile walichokubaliana kwamba pesa za matumizi kwa ajili ya ulinzi angalau zifike asilimia mbili ya mapato jumla ya Taifa yaani GDP kufikia mwaka 2024. Ujerumani pamoja na nchi zingine nyingi bado hazijafikia malengo hayo.

Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Mark Esper, wakati anatangaza uamuzi huo, alisema kwamba hatua hiyo ni sehemu ya mpango wa muda mrefu wa kuhamisha wanajeshi wa Marekani katika eneo hilo.

Alisema: "Ni mkakati muhimu na uhamisho utakao kuwa na manufaa na ambao bila shaka yoyote utasaidia katika kufikia kanuni za msingi za kuimarisha Marekani," alisema Esper.

Hatua hiyo imepangiwa kugharimu serikali ya Marekani dola bilioni kadhaa na pia itapunguza uwapo wa wanajeshi wa Marekani nchini Ujerumani kwa zaidi ya asilimia 25.

"Ndege za kivita zitahamishwa hadi Italia huku baadhi ya wanajeshi huenda wakahamishwa Poland," alisema Esper.

Hata hivyo umauzi huo umekosolewa na maafisa wa Ujerumani, huku mwenyekiti wa kamati ya masuala ya mambo ya nje akisema kuwa hilo huenda likadhoofisha muungano wa NATO.

Mkuu wa Jimbo la Bavaria, Ujerumani, Markus Soeder, alisema anasikitishwa na uamuzi huo. Pia aliishutumu nchi hiyo kwa kuchukua hatua zinazoathiri Marekani kibiashara.

Aidha, alidai uwapo wa majeshi Ujerumani unawafaida kwa sababu wanajeshi hao hufanya manunuzi nchini humo.

Vikosi vya Jeshi vya Marekani nchini Ujerumani ni urithi wa tangu baada ya Vita vya Pili vya Dunia Ujerumani iliposhindwa.

Ujerumani sasa hivi ndio mwenyeji wa idadi kubwa ya wanajeshi wa Marekani waliopo Ulaya, ikifuatiwa na Italia, Uingereza kisha Uhispania.

Baadhi ya maofisa wa Marekani wanaoishi Ulaya pia wanasaidia katika oparesheni za nchi ambazo siyo wanachana na idadi ya wanajeshi wa Marekani inabadilika huku wakihamishwa ndani. **BBC**

HABARI MICHEZO

# RONALDO AZIDIWA KETE NA IMMOBILE



**TURIN,** Italia

MATUMAINI ya Cristiano Ronaldo kumaliza ligi kama mfungaji bora wa Ulaya yameyeyuka baada ya kushindwa kufunga bao wakati timu yake ya Juventus ikichapwa na Cagliari.

Ronaldo amefunga mabao 31 kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, msimu huu lakini usiku wa Jumatano mambo yalikuwa magumu kwake.

Ronaldo anaburuzwa na straika wa Lazio, Ciro Immobile kwa mabao manne katika mbio za kuwania kiatu cha dhahabu Ulaya.

Mshambuliaji huyo alifunga bao lake la 35 msimu huu wakati Lazio wakiichapa Brescia magoli 2-0, hapo Jumatano.

Huku ukiwa umebakia mchezo mmoja Ligi Kuu Italia kumalizika msimu huu, Immobile ndiye anayeongoza kwa kufunga mabao mengi kwenye ligi tano kubwa Ulaya akimzidi bao moja, nyota wa Bayern Munich, Robert Lewandowski, ambaye alimaliza msimu wa Bundesliga akiwa na mabao 34.

Immobile pia amebakiwa na bao moja kufikia rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi kwa msimu mmoja wa Serie A.

Gonzalo Higuain aliweka rekodi ya kufunga mabao 36 wakati akiichezea Napoli msimu wa 2015/16.



# Inter kumsajili jumla Sanchez

**MANCHESTER,** England

INTER Milan inataka kumsajili fowadi wa Manchester United, Alexis Sanchez kwa mkataba wa kudumu.

Mshambuliaji huyo wa Chile mwenye umri wa miaka, 31, amekuwa na msimu wa kuvutia wakati akicheza kwa mkopo nchini Italia na alifunga bao lake la tatu wakati wa ushindi wa Jumamosi wa 3-0 dhidi ya Genoa.

Mkataba wake kule United unamfanya alipwe kiasi cha pauni 400,000 kwa wiki, na kocha Ole Gunnar Solskjaer hana mpango wa kumbakisha kwenye kikosi mchezaji huyo wa zamani wa Barcelona kwa ajili ya msimu ujao.

United haina mpango wa kuendelea na Sanchez na nyota huyo wa zamani wa Arsenal ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2022, anaonekana kufurahia maisha ya Italia.

Na sasa Inter inataka kumbakisha mchezaji huyo ambaye bado anaonekana kurudi kwenye kiwango chake katika mechi za hivi karibuni.

Tangu alipotua Inter, Sanchez alikuwa akikabiliwa na majeruhi ya mara kwa mara hali iliyomfanya kushindwa kupata nafasi ya kucheza mechi nyingi.

Lakini baada ya ligi kurudi kutoka kusimama kwa kipindi cha miezi mitatu kwa mlipuko wa virusi vya corona, Sanchez sasa ameanza kuonyesha ubora wake.

# City yamtaka Torres kuziba pengo la Sane

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City ipo kwenye mazungumzo ya kutaka kumsajili winga wa Valencia, Ferran Torres kwa ada ya euro milioni 23.

Anaweza kuwa usajili wa kwanza kwa City kipindi hiki cha majira ya joto na kuchukua nafasi ya fowadi wa Ujerumani, Leroy Sane, ambaye aliondoka kwa miamba hao wa Ligi Kuu England na kwenda kwa mabingwa wa Bundesliga, Bayern Munich.

Torres, ambaye ana mwaka mmoja uliobaki kwenye mkataba wake na miamba hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, thamani yake ni pauni milioni 40.

BBC Sport inaelewa kwamba, mchezaji huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 20 anataka kwenda pale katika dimba la Etihad.

City, ambao walimaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, pia wanataka kusajili mlinzi wa kati kipindi hiki cha majira ya joto.

Mlinzi wa kati wa England, John Stones mwenye umri wa miaka 26, na beki wa kimataifa wa Argentina, Nicolas Otamendi mwenye umri wa miaka 32, wamenyang'anywa namba na Eric Garcia mwenye umri wa miaka 19 ambaye ana 'upatna' mzuri na Aymeric Laporte.



# Van Dijk amtabiria makubwa Keita

**LIVERPOOL,** England

MLINZI wa Liverpool, Virgil van Dijk ana matumaini kwamba, Naby Keita atakuwa fiti zaidi msimu ujao, baada ya kusumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara na atathibitisha ubora wake.

Keita mwenye umri wa miaka 25, alijiunga na wekundu hao akitokea RB Leipzig mwaka 2018 baada ya kuwa na wakati wa kuvutia kule Ujerumani, ambako alianzia klabu ya Salzburg, alikidumu kwa muda wa miaka miwili hadi 2016.

Nchini Ujerumani, Keita alijijengea jina na kujiweka kama mmoja wa viungo bora zaidi Ulaya wanaochipukia na hivyo kujikuta akiwaniwa na klabu kadhaa za Ulaya.

Liverpool ilimsajili mchezaji huyo kwa pauni milioni 54, lakini misimu yake miwili kwenye Ligi Kuu England imeathiriwa na majeruhi ya mara kwa mara.

Na Van Dijk anaamini kwamba, Keita atakuwa bora zaidi kwa msimu ujao, na atauthibitishia ulimwengu namna gani alivyo na kipaji kikubwa.

"Nina furaha kwa Naby," alisema Van Dijk akiiambia tovuti ya Liverpool.

"Naby ni mtu mzuri, ana bidii na kiwango chake ni cha juu na ni mchezaji wa daraja la juu kabisa.




# ZAHA: NAIOGOPA MITANDAO YA KIJAMII




**LONDON,** England

FOWADI wa Crystal Palace, Wilfried Zaha amebainisha "alikuwa anaogopa" kuingia kwenye mitandao ya kijamii kwa sababu ya ubaguzi wa rangi.

Zaha alikumbwa na zahama ya kubaguliwa mwezi huu na kijana wa kiume mwenye umri wa miaka 12 ambaye alikamatwa na baadaye kuachiwa kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast amesema aliripoti polisi kuwa na akaunti 50 za mitandao ya kijamii.

"Kila mara nilikuwa na hofu na hata nikiangalia kwenye akaunti zangu za nilikuwa na hofu kubwa," amesema akiiambia CNN.

"Kwangu mimi kwa sasa siwezi hata kuingia kwenye ukurasa wangu wa Instagram, kwa sababu hofu yangu kubwa ni maneno ya kibaguzi."

# *Milan, Ibrahimovic waanza mazungumzo*

**MILAN,** Italia

MKURUGENZI wa AC Milan, Ricky Massara amesema kwamba klabu hiyo ya Serie A ipo kwenye mazungumzo na Zlatan Ibrahimovic juu ya mkataba mpya.

Ibrahimovic ameiimarisha Milan tangu alivyotua hapo kwa uhamisho huru Januari, ambapo nyota huyo mwenye umri wa miaka 38 mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu 2019-20.

Mchezaji huyo wa zamani wa Manchester United, Paris Saint-Germain na Barcelona alifunga mabao mawili Jumatano wakati miamba hao wa Serie A wakiibuka na ushindi wa 4-1 dhidi ya Sampdoria, akifikisha mabao 10 kwa mwaka huu 2020.

Alipoulizwa kuhusu majaliwa ya Ibrahimovic, Massara aliiambia Sky Sport Italia: "Tunazungumza na Mino Raiola (wakala wake) na tunajaribu kuhakikisha tunambakiza.

"Kuna vitu ambavyo tunavitathmini pamoja, ukiwamo mkataba wa Ibra na mazungumzo yanaonekana kuwa katika nafasi nzuri.

"Tuna furaha, kwa sababu mazungumzo yetu na Ibra yanakwenda vizuri, na naamini kwamba tunaweza kumbakisha hapa kwa mara nyingine tena."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SPURS YATANGAZA KUMWANIA DIAZ

●●● Ni baada ya kiwango cha winga huyo msimu huu kuimarika na kumvutia Mourinho...

**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho, amesema anataka kumsajili winga wa Porto na Timu ya Taifa ya Colombia, Luis Diaz, ambaye ana umri wa miaka 23, vyombo mbalimbali vimeandika.

**Taarifa zinasema kuwa winga huyo wa kushoto amekuwa akifuatiliwa na kocha wake wa zamani baada ya kufunga mabao 14 na kutoa pasi za mwisho saba.**

Inaelezwa Diaz amekuwa katika kiwango cha kuvutia katika msimu huu wa Ligi Kuu Ureno maarufu Premiere Liga.

Gazeti moja la kila siku la Ureno limeeleza Spurs imeonyesha nia ya kunasa saini ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 23 katika majira ya joto mwaka huu.

Porto ilimsajili nyota huyo kutoka Colombia katika klabu ya Junior kwa ada ya pauni milioni 6.5 Julai mwaka jana na mchango wake uliisaidia kuwafunga mahasimu wao Benfica katika harakati za kuwania taji la ligi.

Winga huyo pia anatakiwa na Zenit St Petersburg, lakini wachezaji wenzake wa Ureno, Radamel Falcao na James Rodriguez walimshawishi kuichagua klabu hiyo ya nchini Ureno.

Inaonekana kama Mourinho ametengewa bajeti finyu na mabosi wa klabu hiyo baada ya Spurs kushindwa kumaliza kwenye nafasi nne za juu katika Ligi Kuu England.

Kocha huyo anataka kusajili wachezaji wapya watano ili kukiimarisha kikosi chake ifikapo dirisha la usajili la majira ya joto wakiwamo nyota wa Southampton, Pierre Emile Hojbjerg na Callum Wilson wa Bournemouth.

Tayari Spurs imeshamkosa Jan Vertonghen ambaye ameondoka klabuni hapo baada ya mkataba wake kumalizika huku straika chipukizi, Troy Parrot akikaribia kujiunga kwa mkopo na Millwall inayoshiriki Ligi ya Championship kwa sababu ya kwenda kupata uzoefu na namba kwenye kikosi cha kwanza.

## ZISIKUPITE

### ALABA KUIKAMUA BAYERN

WAKALA wa beki anayewindwa na Manchester City pamoja na Paris St-Germain, David Alaba ameiambia Bayern Munich itoe pauni milioni 18 ili kupata saini ya mwaka mmoja zaidi ya nyota huyo. ***(Bild - in German)***

### LIVERPOOL, CITY VITANI

LIVERPOOL na Manchester City zote zimeonyesha nia ya kumsajili beki wa Sevilla na Timu ya Taifa ya Brazil, Diego Carlos, ambaye dau lake lililoko kwenye mkataba wake ni pauni milioni 70. ***(Star)***

### AUBAMEYANG KITAELEWEKA

HATIMA ya straika wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang kuendelea kubakia katika klabu hiyo itajulikana baada ya fainali ya Kombe la FA, huku Barcelona na Inter Milan zikiendelea kumfuatilia nyota huyo mwenye umri wa miaka 31. ***(Mirror)***

### HENDERSON AJIPANGA

MAZUNGUMZO kati ya Manchester United na golikipa wake, Dean Henderson (23), ambaye msimu huu alikuwa kwa mkopo katika klabu ya Sheffield United yako kwenye hatua za mwisho. ***(Sky Sports)***

### CHILWELL AIVURUGA CHELSEA

CHELSEA imemtaja beki wa kushoto wa Leicester City, Ben Chilwell (23), kuwa ni mchezaji wake namba moja itakayemsajili pamoja na beki wa Ajax, Nicholas Tagliafico ambaye ana umri wa miaka 27. ***(Goal)***

### MANNING SOKONI

WEST Ham United imeonyesha nia ya kumsajili beki wa Queens Park Rangers na nyota wa zamani wa Timu ya Taifa ya vijana ya Jamhuri ya Ireland (U-21), Ryan Manning, 24. ***(Telegraph - subscription required)***

### ARSENAL MAMBO MAGUMU

ATLETICO Madrid imekacha ofa iliyoboreshwa ya pauni milioni 22.6 pamoja na kupewa kiungo Mfaransa, Matteo Guendouzi kutoka kwa Arsenal kumuuza kiungo wake Mghana, Thomas Partey (27). ***(AS - in Spanish)***

### HART MAMBO SAFI

GOLIKIPA wa zamani wa Burnley, West Ham na Manchester City, Joe Hart (33), anakaribia kukamilisha mchakato wa kujiunga na klabu ya Celtic inayoshiriki Ligi Kuu ya Scotland. ***(Sun)***

### HULK AITAMANI EPL

MSHAMBULIAJI Mbrazil, Hulk (34), ameweka wazi anapenda kujiunga na klabu inayoshiriki Ligi Kuu England baada ya mkataba wake na Shanghai SIPG utakapomalizika Januari, mwakani. ***(Talksport)***

### KLAIBER KUTUA LEEDS

LEEDS United ambayo imerejea Ligi Kuu England inataka kumsajili beki wa FC Utrecht, Sean Klaiber (25) kuimarisha kikosi chake. ***(Voetbal International - in Dutch)***

### BRAITHWAITE KUACHWA

BARCELONA inajipanga kumtema nyota wake mpya, Martin Braithwaite (29), kutokana na mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Denmark kutokuwa kwenye mipango ya kocha, Quique Setien kwa ajili ya msimu ujao. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

## HABARI MICHEZO



Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo (kulia), akielezea uzinduzi wa tamthilia mpya iitwayo 'Karma' itakayoanza kurushwa hewani kesho. Wengine katika picha ni Wema Sepetu (wa pili kulia), Max Ryoba na mzalishaji wa tamthilia hiyo, Neema Ndepanya (kushoto). **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wema Sepetu aing'arisha Karma

**Na Mwandishi Wetu**

BURUDANI inaendelea! Chaneli ya Maisha Magic Bongo (MMB) iliyoko katika king'amuzi cha DSTV imezindua tamthilia mpya iitwayo 'KARMA', imeelezwa.

Tamthilia hiyo itaanza kuonekana ramsi kuanzia kesho na inatarajiwa kuwa gumzo nchini kutokana na kuhusisha waigizaji nguli huku ikiwa na visa na mikasa kedekede yenye lengo la kuhakikisha watazamaji wanapata burudani.

Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo, alisema kitendo cha MMB kuzindua tamthilia hiyo mpya kinaendana na azma ya chaneli yao kuhakikisha watazamaji wake hawapungukiwi na burudani zenye asili ya Kitanzania kwa kuigizwa na wasanii wa hapa nchini.

Shelukindo alisema lengo la kampuni yao ni kuwapa fursa wasanii wa hapa nchini kujitangaza kimataifa na vile vile kupeperusha jina la Tanzania kwa kuandaa kazi zenye viwango bora.

Awali Mkuu wa Chaneli ya MMB, Barbara Kambogi, aliwataja baadhi ya wasanii waliohusika katika kuandaa tamthilia hiyo ni pamoja na Neema Ndepanya ambaye ni mwandishi wa tamthilia maarufu ya SARAFU.

Kambogi pia alimtaja Miss Tanzania (2006), Wema Sepetu, ambaye ameigiza katika filamu nyingi kwa umahiri ikiwamo iitwayo A point of no return naye ameshiriki kuigiza katika tamthilia hiyo ya Karma.

Akizungumza katika uzinduzi wa tamthilia hiyo, Wema alisema Karma inaangazia zaidi 'kinadada' wawili ambao ni wapinzani wa jadi waitwao, Suzanne na Veronica, ambao wote wanafanya kazi serikalini na wanaheshimika kwenye jamii.

Alisema ndani ya tamthilia hii kuna visa na mikasa ya mahaba, siri nzito, siasa na visasi na yeye ameigiza kama daktari (Dr. Desire), ambaye anajikuta katika vita vya kisiasa na Veronica katika mchuano wa uchaguzi mkuu, jambo ambalo liliongeza hamasa kwenye tamthilia hiyo.

# Coastal Union yaanza mipango

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Coastal Union umesema hauna wasiwasi wowote kutokana na tetesi za nyota wake waliokisaidia kikosi hicho kufanya vema msimu huu, kutakiwa na klabu nyingine zikiwamo vigogo, Simba na Yanga.

Mwenyekiti wa Coastal Union, Steven Mguto, aliliambia gazeti hili hawana presha kwa sababu wana benchi la ufundi imara ambalo linaweza kuwatengeneza wachezaji wengine na timu yao ikaendelea kufanya vema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.



Mguto alisema tetesi hizo wamezisikia lakini watawaruhusu wachezaji wao kuondoka baada ya klabu zinazowahitaji kukubali kuwalipa kiasi cha fedha wanazotaka.

Kiongozi huyo alisema hawatamzuia mchezaji yoyote kuondoka kama klabu inayomhitaji itakubali kumpatia maslahi bora kwa ajili ya kuendeleza kipaji cha mchezaji husika pamoja na wao ambao wamemkuza nyota huyo.

"Viongozi tulikutana na kujadili suala hilo baada ya kusikia na kuona tetesi juu ya wachezaji wetu, kwa sasa tunachokisubiri ni ripoti ya kocha wetu (Juma Mgunda), tutaangalia wachezaji ambao wanabaki na wale ambao wanaondoka, iwe kwa sababu ya kutakiwa na timu nyingine, halafu tutaanzia hapo."

Aliongeza wamepanga kuanza maandalizi ya msimu ujao mapema na hivyo wamemtaka Mgunda kuwasilisha ripoti yake mapema ili ifanyiwe kazi kwa ufanisi.

# MBIVU, MBICHI LIGI KUU Z'BAR KUJULIKANA KESHO

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BINGWA wa Ligi Kuu Zanzibar msimu wa 2019/20 anatarajiwa kujulikana kesho baada ya kumalizika kwa mechi tano zitakazochezwa kwenye viwanja mbalimbali visiwani hapa, imeelezwa.

Mshindi wa ligi hiyo ndio ataiwakilisha Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Pia timu moja itakayoungana na nyingine tano zilizoshuka daraja itafahamika kesho jioni.

Akizungumza na gazeti hili, Mkurugenzi wa Mashindano wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Ali Mohamed Ameir, alisema maandalizi kuelekea michezo hiyo yamekamilika na wanaamini klabu zitapambana kuhakikisha timu bora inanyakuwa ubingwa.

Ameir alisema ZFF kwa kushirikiana na wasimamizi wake maalum watafuatilia michezo yote kwa karibu ili kuhakikisha vitendo vya upangaji wa matokeo havitokei tena kwenye ligi hiyo.

"ZFF kupitia Kamati ya Mashindano imejipanga kuhakikisha vitendo vyoyote vya upangaji wa matokeo havitatokea katika michezo hiyo muhimu, vilabu vinatakiwa kufahamu na kujiepusha kutenda kosa hilo na kutakiwa kuwa tayari kukabiliana na ushindani ili kumpata bingwa atakayeiwakilisha vema Zanzibar," alisema.

Aliitaja mechi zitakazochezwa kesho ni kati ya Chuoni dhidi ya Polisi, KMKM dhidi ya Mafunzo, JKU itawakaribisha Malindi huku Mlandege akiwavaa Jang'ombe Boys na Kipanga itawafuata Zimamoto.

Vita ya kuwania ubingwa wa ligi hiyo iko kati ya Mlandege, JKU na Zimamoto.

## Straika Mbao awaonya Ihefu

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA hatari wa Mbao FC, Waziri Junior ameionya Ihefu FC kuacha kushangilia wamepanda Ligi Kuu Tanzania Bara, kwa sababu anaamini mechi ya marudiano itakuwa ngumu kuliko mechi nyingine walizowahi kucheza msimu huu.

Waziri ambaye amemaliza Ligi Kuu Bara akiwa na magoli 13, alisema hayo mara baada ya timu yake kunyukwa mabao 2-0 Uwanja wa Highland Estate, Mbalizi, Mbarali jijini Mbeya na kuwaweka kwenye nafasi ngumu ya kusalia kwenye Ligi Kuu.

Mbao itaikaribisha Ihefu katika mechi ya marudiano itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza na mshindi wa jumla atashiriki Ligi Kuu Bara msimu ujao.

Mabao ya Ihefu katika mechi ya kwanza ya mtoano yalifungwa na Steven Mwaijala kwa njia ya penalti dakika ya nne na Mridi Tangai dakika ya 84.

Naye Kocha Mkuu wa Ihefu, Maka Malwisi alisema amejiandaa kikamilifu na mechi ya marudiano baada ya kuanza vema hatua hiyo ya mtoano.

Michezo
Ijumaa Julai 31, 2020
Nipashe



Spurs yatangaza kumwania Diaz UKURASA 22




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa, Tarimba Abbas (kushoto), akimkabidhi tuzo ya Mchezaji Bora, kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Feitoto', baada ya kuibuka mshindi wa shindano lililoendeshwa na kampuni hiyo kwa timu ya Yanga kwa msimu wa 2019/20 wa Ligi Kuu Tanzania Bara. **PICHA: MTANDAO**

## Simba SC yatangulia mapema Rukwa

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kiliwasili salama Sumbawanga Mjini jana jioni tayari kwa mchezo wa fainali ya Kombe la FA dhidi ya Namungo FC, utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela.

Simba imewasili Sumbawanga ikitokea jijini Mbeya ilipoweka kambi ya siku tatu kujiandaa na mchezo huo wa kufunga msimu wa mwaka 2019/20.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, aliliambia gazeti hili wachezaji wote wako katika hali nzuri na leo asubuhi walitarajia kufanya mazoezi kuendelea kujiimarisha kwa ajili ya fainali hiyo.

Rweyemamu alisema wanahitaji kukamilisha msimu kwa furaha kama walivyoanza kwa kuchukua Ngao ya Jamii. Simba ilitinga fainali ya michuano hiyo baada ya kuwafunga Yanga mabao 4-1 wakati Namungo yenyewe ilifika hatua hiyo kwa kuwaondoka Sahare All Star ya jijini, Tanga.

Tayari Simba ilishakata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Namungo yenyewe hata ikifungwa, itakwenda kuiwakilisha Tanzania Bara kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

# Tshishimbi aitingisha Yanga

## ●●● Uongozi wa klabu hiyo wakiri kushindwa kumpa dau alilohitaji, yamweleza uamuzi ni...

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kiungo na nahodha wa Yanga, Papy Tshishimbi, kusema bado hajasaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia timu hiyo, mabosi wake wameweka wazi wametoa siku 14 kwa Mkongomani huyo kufanya uamuzi kuhusu hatima yake.

**Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam jana zinaeleza Yanga imemtaka mchezaji huyo kufanya uamuzi ndani ya muda waliompa na endapo atakuwa kimya, watakuwa wameachana naye rasmi.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Wakili Patrick Simon, alikiri kuwa kiungo huyo bado hajasaini mkataba mpya ila klabu na mchezaji huyo ilifikia katika hatua nzuri za mazungumzo.

Simon alisema Yanga ilipenda kuendelea kupata huduma ya Tshishimbi, lakini itakuwa tayari pia kuheshimu uamuzi ambao ataufikia baada ya kutafakari ofa ambayo wamempatia nyota huyo.

"Alifanya mazungumzo na makubaliano yalifikiwa, bado tu kusaini mkataba mpya, baada ya mazungumzo hayo, Hersi Said (GSM) alitueleza viongozi, lakini uongozi wa klabu nao ulitoa mapendekezo yake juu ya kiasi anachokitaka Tshishimbi na tulisema tukipunguze," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kuwa uongozi ulimpatia mkataba, lakini nyota huyo ambaye aliwahi kutajwa kutakiwa na Simba, hakuwa tayari kusaini kwa sababu ya kutofikia mahitaji yake.

Alisema Tshishimbi alihitaji kupewa dau kubwa zaidi pamoja na mahitaji mengine ambayo kwa sasa Yanga haina uwezo wa kumpatia.

"Sasa jukumu lipo kwake ikiwa ataridhika na mkataba tuliompa, atasaini mkataba, lakini nikiri tu kuwa bado hajasaini mkataba mpya hadi leo (jana)," Wakili Simon alisema.

Alieleza Yanga ni taasisi kubwa na hakuna mchezaji au kiongozi ambaye yuko juu ya klabu hiyo, huku akisisitiza kazi zote zinafanywa kwa kufuata taratibu.

"Suala la mikataba ya wachezaji sio tu Tshishimbi, wapo wachezaji wengine ambao bado hawajasaini mkataba mpya, tumepanga kukutana nao Jumatatu (Agosti 3, mwaka huu), hatuwezi kupoteza muda mwingi kwa mchezaji mmoja ambaye amepewa mapendekezo ya mkataba wetu tayari," aliongeza.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela, alisema bado wanamwitaji mchezaji huyo na sasa uamuzi wa kuendelea kubakia Jangwani umebakia katika upande wake.

"Kila siku tulikuwa tunafanya mawasiliano naye na kufika kwenye makubaliano mazuri, tukawa tunasubiri kitendo cha kusaini mkataba, ila pia naye tulimpa nafasi ya kumsikiliza," alisema Mwakalebela.

Mechi ya mwisho Tshishimbi kuitumikia Yanga ilikuwa ni ya hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA, dhidi ya watani zao Simba ambayo walitolewa katika michuano hiyo baada ya kupokea kichapo cha mabao 4-1.

Ilidaiwa nyota huyo alicheza mchezo huo akitoka kuwa majeruhi na taarifa za ndani zinadai bado hajawa fiti kwa asilimia mia moja.

Tshishimbi amekuwa mchezaji wa pili 'kuivuruga' Yanga katika mchakato wa kusaini mkataba mpya baada ya kiungo mshambuliaji wake, Bernard Morrison kutangaza kutoutambua mkataba mpya wa miaka miwili ambao utamweka ndani ya timu hiyo hadi mwaka 2022.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >